# Nipashe

Jumamosi Februari 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580497

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Meneja** TANESCO kortini madai ya uhujumu uchumi

UKURASA 3



**Washtakiwa** dawa za kulevya waachiwa huru

UKURASA 5

**Sarri awapiga vijembe Juventus, Ronaldo**

UKURASA 21

# Magufuli atangaza maombi siku tatu

• **Kwa** ajili ya maradhi tishio, afichua Kijazi alivyozuia watu kutumbuliwa, aanika walichoteta na Maalim Seif... *Endelea ukurasa 2 & 3*




Rais Dk. John Magufuli akiongoza waombolezaji kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Mhandisi John William Kijazi, katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## HESLB yataja sababu deni la mtumishi wa TANESCO

UKURASA 3



## ...Ashangaa Dk. Mpango kuzushiwa kifo

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store


**MICHEZO** SIMBA YAITANGAZIA AL AHLY 'TOTAL WAR' UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiitikia dua ikisomwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi (kulia kwake), baada ya kumalizika kwa Sala ya Ijumaa katika Msikiti wa Miembeni, Wilaya ya Mjini Unguja jana. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Mustafa Kitwana. **PICHA: IKULU**

## ...Ashangaa Dk. Mpango kuzushiwa amefariki

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli, amesoma ujumbe mfupi wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliomtumia akiwa hospitalini, huku akielezea kusikitishwa na vitendo vya kutishana na uzishi ikiwamo taarifa kuwa waziri huyo amefariki dunia.

Ujumbe huo alimtumia ikiwa siku moja baada ya baadhi ya watu kumzushia kupitia mitandao ya kijamii kuwa amefariki dunia wakati yuko hai na anaendelea vizuri na matibabu.

Ujumbe huo wa Dk. Mpango ambao alimtumia Rais, aliusoma jana wakati wa misa ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, aliyefariki dunia juzi.

"Niwaombe Watanzania matatizo yoyote yanayotokea yatufanye kuwa wamoja zaidi. Hofu ni mbaya, tumtangulize Mungu pamoja na juhudi zingine.

"Unapoona kitu huwezi kukitatua wewe mwambie Mungu ndiye muweza. Lakini tumefikia mahali tunatishana sana. Leo (jana) asubuhi nimetumiwa ujumbe mfupi na Waziri wa Fedha, Dk. Mpango, ambaye amelazwa Dodoma ninaomba niusome hapa kwa faida ya wale waliokuwa wana 'tweet' kwamba amekufa. Baba Paroko naomba uniruhusu tu," alisema.

"Mheshimiwa Rais asante sana nimepata ujumbe wako kupitia kwa mke wangu. Kwa neema ya Mungu ninaendelea vizuri. Ninakula na ninafanya mazoezi ya kifua na kutembea. Hao wanaonizushia kifo kwenye mitandao, niliwaombea msamaha kwa Yesu wakati wa sala ya jioni jana (juzi).

"Mheshimiwa Rais, Mungu akubariki na akupe neema na ujasiri zaidi katika kuliongoza taifa letu katika wimbi hili. Naungana nawe na familia katika maombolezo ya kifo cha mpendwa wetu Mheshimiwa Katibu Mkuu Kiongozi, John Kijazi. Rest in peace (pumzika kwa amani)," mwisho wa nukuu yake.

# JPM atangaza siku tatu za maombi

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametangaza siku tatu za kufunga na kuomba dhidi ya magonjwa yaliyoikumba dunia, ukiwamo ugonjwa wa corona na kuwaeleza Watanzania kuwa Mungu ndiye muweza na ataisimama na Tanzania.

Alitangaza maombi hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa misa ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, aliyefariki dunia juzi jijini Dodoma.

Rais alisema Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakari Zuberi, alimweleza kuwa Waislamu wametangaza muda wao wa kuomba ambao walifanya hivyo jana.

"Niwaombe tena Watanzania kama kuna mahali tuliteteleka tuendelee kumwomba Mungu. Tuanze leo (jana) na ndugu zetu Waislamu wameshaanza, kesho (leo) kwa ndugu zetu Wasabato na Jumapili kwa ndugu zetu Wakristo. Tuombe kwa siku tatu kwa kuomba na kufunga, nina uhakika tutashinda.

"Nataka kuwapa nguvu hiyo ndugu zangu Watanzania, tutahangaika sana Mungu ndiye mwenye uwezo wa kila kitu. Niwaombe viongozi wa dini endeleeni kuhimiza maombi tutashinda. Tulishinda mwaka jana, tutashinda mwaka huu, tutashinda miaka yote. Kamwe Mungu hajaliacha taifa hili," alisema.

Rais Magufuli alisema mwaka jana taifa lilishinda mpaka likaingia kwenye uchumi wa kati na corona ilikuwapo na miradi mingi ikaendelea kutekelezwa wala hawakujifungia.

"Hata sasa hatutaweka lock down (kujifungia) kwa sababu tunajua Mungu yupo siku zote," alisisitiza na kuongeza kuwa ameona atoe wito huo kwa sababu anaamini kuwa yeye ndiye kiongozi na ana wajibu wa kukumbusha kwamba taifa liko mikononi mwa Mungu na ataendelea kusimama.

"Ninachotaka kusema Watanzania, magonjwa yapo na yataendelea kuwapo, magonjwa ya vifua, ya kupumua na kadhalika yatakuwapo na hayakuanzia hapa. Ziko nchi zimepoteza watu wake wengi. Tanzania Mungu ametusaidia sana kipindi cha mwaka uliopita," alisisitiza.

Rais Magufuli aliwataka Watanzania waendelee kusimama na kuchukua tahadhari kwa kumtanguliza Mungu kwa sababu hashindwi.

Alisema kama Tanzania ilishinda mwaka jana inawezekana hili ni jaribu lingine nalo ambalo wakisimama na Mungu watashinda na kutaka wasitishane na kuogopeshana.

"Kufa tutakufa tu unaweza ukafa na malaria, saratani ukafa kwa magonjwa mengine, kwa sababu kufa kupo kamwe tusimuache Mungu huo ndio wito wangu."

### AMWELEZEA KIJAZI

Rais Magufuli alisema wakati amechaguliwa na Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, mwaka 1995, alitembelea maeneo mengi ya barabara ndipo alipoutambua utendaji kazi wa Balozi Kijazi wakati huo akiwa Dodoma.

"Nilimwuliza kwa nini barabara zake za mikoa zote ni nzuri wakati fedha zinazotolewa ni sawa, akasema anachofanya kuhakikisha kila senti inayotolewa na serikali inatumika kwa kusimamia kikamilifu makandarasi fedha alizokuwa anazopelekewa zilikuwa kidogo ikilinganishwa na wenzake," alisema.

Rais Magufuli alisema utendaji wa Balozi Kijazi ulimfanya aliporudi wizarani, alimwomba waziri wake wakati huo alikuwa ni Anna Abdallah, ampandishe kuwa mkurugenzi ili asimamie barabara zote zinazofanyiwa matengenezo na alikubali.

"Mwaka 2000 baada ya uchaguzi nilichaguliwa kuwa Waziri, nikaenda Ikulu nikamuona Rais Mkapa amchagua Kijazi kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, hakunipa jibu naona alinishangaa, mwaka 2002 akateuliwa kwenye nafasi hiyo, alifanya kazi kweli na mabadiliko mengi yalifanyika na kutengenezwa barabara nyingi," alisema.

Alisema baada ya miaka mitano, Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete alimwona na kumteua kuwa Balozi ambaye alikwenda India kuiwakilisha Tanzania na aliwezesha kuwapo ukaribu baina ya nchi hizo hadi Waziri Mkuu wa India, alikuja nchini.

"Nilipoteuliwa Rais, nilimwona Balozi Kijazi anafaa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Alikuwa mnyenyekevu hajikwezi, ananizidi umri amezaliwa mwaka 1956, mimi mwaka 1959, ukimwita Balozi Kijazi alikuwa mnyenyekevu sana, hakuwa na makuu.

"Saa nyingine ulikuwa ukitaka kumtumbua mtu mwingine anakwambia labda ungesubiri hata siku mbili ajirekebishe umwangalie. Kweli ukikaa siku mbili unakuta amebadilika. Iko mifano sitaki kuitoa hapa wapo watu hapa wamebaki kwa sababu ya Balozi Kijazi," aliongeza.

Alisema Balozi alikuwa akiweka mambo sawa na wakati wa kuchambua miswada iliyokuwa ikitoka kwa makatibu wakuu, aliichambua vizuri na kulifanya Baraza la Mawaziri lisipate shida.

"Tumepoteza mtu muhimu, alizaliwa mwaka 1956 hadi leo alikuwa Katibu Mkuu Kiongozi maana yake ilipofika mwaka 2017, nilijaribu kutafuta wa kumrithi ninakosa, nikamwongeza miaka miwili. Nikifikiri baada ya miaka miwili nitapata mwingine, ikaisha 2019 sikupata nikamwongeza tena miaka miwili, Mungu akasema umezoea ngoja akamtumie mwenyewe," alisema.

Rais Magufuli alisema Balozi Kijazi alikuwa hakosi kanisani, mkarimu, hajioni, aliwatumikia kwa sawa watu bila kujali rika na kwamba kifo chake ni pengo kubwa. Katika misa ya kuuaga mwili wa Balozi Kijazi, viongozi wengine waliohudhuria ni Mstaafu wa Awamu ya Nne, Kikwete; Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu Kassim Majaliwa; Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma.

Wengine ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, Mawaziri, Makatibu Wakuu wa Wizara, viongozi wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Aboubakar Kunenge.


## TANGAZO LA MNADA

**TAN-GLOBAL VENTURES COMPANY LIMITED** kwa idhini iliyopewa na **NATIONAL BANK OF COMMERCE (NBC)** itauza kwa mnada wa hadhara nyumba zilizo orodheshwa kwenye jedwali kwa maeneo na tarehe tajwa hapo chini:

| JINA LA MDAIWA | NAMBA YA KIWANJA/KITALU | ENEO LILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| BAHATI SENGELEMA MANYAMA | CT No. 24768- LO No. 388664 PLOT No. 353, Block "E" HIGH DENSITY, MAJENGO, KAHAMA | MAJENGO - KAHAMA | 15/03/2021 |
| MINYARO LUSHANGA SHIJA | CT No. 23700 – LO No. 388591 PLOT No. MBULU AREA KAHAMA DISTRICT. | MBULU-KAHAMA | 17/03 2021 |
| JUSTINE WEREMA MARWA | CT No. 25321 – LO No. 366528 PLOT No. 507, Block "G" BOMANI AREA, TARIME | BOMANI TARIME | 22/03/2021 |
| JULIUS.M. NTAGERA | CT NO 31622 – LO No. 366714 PLOT No. 28, Block "F" HIGH DENSITY, NYAMWAGA ROAD | NYAMWANGA TARIME | 24/03/2021 |
| EMMANUEL GODWIN GAMBI | CT NO 114905 – LO No. 395223 PLOT No. 68, Block Q, KIBAMBA DAR ES SALAAM | KIBAMBA DAR ES SALAAM | 29/03/2021 |
| BUPE .B. HULILO | CT NO 59922 PLOT NO. 438 Block "B" MBEZI LUGURUNI-DAR ES SALAAM | MBEZI LUGURUNI DAR ES ASALAAM | 31/03/2021 |
| JUMA ABDALLAH SADICK | PLOT NO. 11 TUANGOMA AREA, TEMEKE MUNICIPALITY DAR ES SALAAM CITY | TUANGOMA, TEMEKE - DAR | 2/4/2021 |
| ALLY MOHAMED KAMPUNDA | CT NO. 1760- LO NO. 314106 PLOT NO. 239 BLOCK "DD" MTANDA AREA, LINDI TOWNSHIP | MTANDA AREA LINDI | 12/4/2021 |
| SIMON KISHIWA MALEKELA | CT NO. 78324, LO NO. 277801, PLOT NO. 933, BLOCK "N" KIHONDA AREA MOROGORO MUNICIPALITY | KIHONDA AREA MOROGORO | 14/04/2021 |

**MASHARTI YA MNADA:**

Mnunuzi aliyeshinda anatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano(25%) mara tu baada ya mnada kufungwa,na atakamilisha asilimia sabini na tano(75%) baada ya siku kumi na nne(14),Fedha hiyo isipolipwa ndani ya muda huo mnada utarudiwa bila kurudishiwa fedha ya awali.
ABRAHAM SHEMPEMBA
Mkurugenzi Mtendaji

**Imetolewa leo tarehe 20/02/2021 na TAN-GLOBAL VENTURES CO.Ltd, S.L.P 612, TANGA, abrahamshempemba@gmail.com 0715-752205, 0714-560080, 0692-693410**

HABARI KITAIFA

# Rais aweka bayana walichoteta na Maalim Seif

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli afunguka kuhusu mazungumzo yake na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, yaliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam na Chato, huku kikubwa akihubiri umoja na amani.

Maalim Seif alifariki dunia Alhamisi wiki hii katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na kuzikwa jana kijijini kwao Mtambwe, kisiwani Pemba.

Akizungumza jana katika ibada ya kuaga mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, iliyofanyika viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam, Rais Magufuli alianza kwa kutoa pole kwa familia na taifa kuhusiana na vifo hivyo.

Rais Magufuli alisema wakati wa mazishi ya Maalim Seif, aliwatuma Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, kumwakilisha katika mazishi yake huku akimwelezea kuwa alikuwa kiongozi wa tofauti.

"Mwaka 2015 nilipoingia kuwa Rais na baada ya uchaguzi wa Zanzibar wa marudio, Maalim Seif aliniandikia barua ya kuomba kuja kuniona. Nilisita kidogo kwa nini anataka kuja kuniona wakati hata kwenye uchaguzi hakushiriki.

"Aliandika barua ya pili na baadaye ya tatu. Kila nilipojaribu kupata ushauri kutoka Zanzibar waliniambia nisubiri kwanza, lakini niliamua kumuona. Alikuja Ikulu Dar es Salaam, nilipoanza kuzungumza naye niliona tofauti sana na picha ilivyojengeka, mazungumzo yetu yalikuwa mazuri sana," alisema.

Rais Magufuli alisema katika mazungumzo hayo, Maalim Seif alimweleza kuwa hakushiriki uchaguzi wa pili na alimhakikishia Zanzibar itakuwa salama kwa kuwa hatahamasisha fujo yoyote.

"Alinieleza kuwa miaka yote mitano aliyechaguliwa ataendelea vizuri kutawala. Kauli hii niliiona miaka yote mitano," Rais Magufuli alisema.

"Alinieleza kuwa anapenda amani na angependa Zanzibar na Watanzania wote wakae kwa amani. Kauli hii nilithibitisha kwa vitendo. Ulipotokea uchaguzi mwingine bado alishiriki Serikali ya Umoja wa Kitaifa na mara ya mwisho alikuja Chato na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Alli Mwinyi, na mazungumzo yake yalikuwa ya raha sana.

"Akanipa historia nzuri wakati alipokuwa CCM kwa wakati huo ikiwa TANU (Tanganyika African National Union) na akaniambia alishawahi kufika Chato wakati huo akihamasisha TANU," aliongeza.

Alisema Maalim Seif alikuwa mcheshi na siku zote hata katika ziara ya Chato alihubiri umoja wa Wazanzibar na Watanzania, kitu ambacho amemaliza nacho.

"Tumshukuru Mungu kwamba Maalim Seif amemaliza salama na dhamira yake ya kuujenga umoja na amani ya Wazanzibar na Watanzania, Mungu ampokee mahali pema huko aliko, ni matumaini yangu kwa Wazanzibar na Watanzania tutaendelea kuenzi yote mema aliyoyafanya hasa katika kujenga umoja na amani kwa Wazanzibar na Watanzania," alisema.

## HESLB yataja sababu mtumishi wa TANESCO kuandikiwa deni la milioni 18/-

**Na Thobias Mwanakatwe**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), aidha, imetaja sababu za mtumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Eladi Lugayelukamu, kuandikiwa deni la Sh. milioni 18 wakati hakuwa mnufaika wa mkopo.

Wakati ikitaja sababu hizo, HESLB imesema imepokea namba ya akaunti benki ya mtumishi wa TANESCO, Wilaya ya Biharamulo, mkoani Kagera kwa ajili ya kumrejeshea fedha alizokuwa amekatwa kimakosa.

Mkuu wa Mawasiliano HESLB, Omega Ngole, alisema hayo juzi wakati akihojiwa na ICON TZ online TV kuhusu hatua zilizochukuliwa na bodi hadi sasa katika kumrejeshea fedha mtumishi huyo.

Ngole alisema ni kweli mtumishi huyo baada kubaini anakatwa fedha katika mshahara wake, aliiandikia barua bodi kwamba anakatwa kimakosa wakati hajawahi kuomba mkopo HESLB.

"Tulipopata barua yake miaka miwili iliyopita, tulimjibu kwamba ili tumrudishie fedha zake, atuletee namba ya akaunti ya benki yake pamoja na jina na taarifa zingine kwa kuwa hatuwezi kulipa kwa fedha taslimu," alisema.

Ngole alisema katika hali ya kushangaza, mtumishi huyo hakuwahi kupeleka akaunti HESLB kama alivyotakiwa hadi juzi Meneja wa HESLB Mwanza alipomkumbusha ndipo akazipeleka na sasa taratibu za kumwandalia malipo zinaandaliwa.

Ngole alifafanua kuwa kilichotokea hadi mtumishi huyo akawa anakatwa kimakosa, ni kwamba HESLB ilipeleka bili ya mnufaika wa kweli ambaye ameajiriwa TANESCO, lakini kulitokea tatizo la mawasiliano akawa anakatwa mtumishi ambaye si mnufaika na baada ya kugundua, alisitishiwa makato.



Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akifungua maji ili kuhakikisha kama yanatoka, wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya maji wilayani Kwimba, Mkoa wa Mwanza. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## Kigogo TANESCO mahakamani kwa madai ya uhujumu uchumi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tabora, imewapandisha kizimbani maofisa waandamizi wawili wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa mashtaka saba likiwamo uhujumu uchumi.

Walipandishwa kizimbani ni aliyekuwa meneja wa TANESCO Mkoa wa Tabora, Mohamed Abdallah, na mhandisi wake, Melkiad Msigwa. Miongoni mwa mashtaka hayo ni kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 60.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Tabora mbele ya Hakimu Tausi Mongi. Waendesha mashtaka, Matereus Maranda na Simon Mashingia, walidai mahakamani hapo kuwa washtakiwa walitenda makosa hayo kati ya Desemba, 2015 na Novemba, 2018 ikiwamo kuendesha genge la uhalifu.

Walidai kuwa Msigwa alighushi risiti kuonyesha kuwa amenunua vifaa mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kituo cha kupozea umeme kwenye mizani ya Puge wilayani Nzega.

Maranda alidai kuwa kati ya Mei 10, 2016 na Juni 23, 2016, katika Manispaa ya Tabora, akiwa mtumishi wa TANESCO Mkoa wa Tabora, alighushi risiti zenye namba 08645 na 0078 kuonyesha kuwa ni nyaraka halali kwa ajili ya kununua vifaa vya umeme huku akijua si kweli.

Aliendelea kudai kuwa katika tarehe zisizojulikana mwaka 2016, Msigwa akiwa Manispaa ya Tabora kwenye ofisi za TANESCO, aliwasilisha nyaraka zilizoghushiwa kutoka Lesheya Investment Company Limited na Soko Electrical Traders kuonyesha kwamba vifaa vilivyoorodheshwa kwenye risiti namba 08645 na 0078 vilinunuliwa na Sinohydro Corporation Limited na kwamba nyaraka hizo ni halali huku akijua si kweli.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa Abdallah kwa nyakati tofauti, kati ya Machi, 2016 na Mei, 2018, akiwa Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tabora, alitumia madaraka yake vibaya na kufanya ununuzi katika mradi ujenzi wa usambazaji umeme kwenye mizani ya Puge kazi ambayo tayari iliidhinishwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) ifanywe na M/S Mawenjeni Electrical Contractor na kujipatia manufaa yasiyo halali ya Sh. 20,492,600.72.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa kwa pamoja na wanakabiliwa na makosa saba yakiwamo ya kuendesha genge la uhalifu kinyume cha aya ya 4 (1) ya jedwali la kwanza pamoja na vifungu vya 57 (1) na 60 (2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200, marejeo ya mwaka 2019, kughushi kinyume cha vifungu vya 333, 335 (a) na 337 vya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16, marejeo ya 2019.

Washtakiwa wote wawili wamepelekwa rumande hadi Machi 4, mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi ya aina hiyo ambayo imeangukia kwenye makosa ya uhujumu uchumi.

# Bei nyama mnadani kuuzwa kwa vipimo

Na Romana Mallya

WAZIRI wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema kuanzia sasa minada ya nyama inayojengwa itakuwa na mizani ili kuondokana na upangaji wa bei kwa kukadiria kwa macho na kumnyima faida mfugaji.

Aliyasema hayo jana alipokutana na wafugaji wa kuku wa nyama, wauzaji wa vifaranga na vyakula ili kusikiliza kero ambazo mojawapo walitaja ni kukosa faida kutokana na mauzo ya kuku kwa sababu ya kuuzwa kwa kukadiriwa kwa macho.

Katika kero hiyo, wafugaji hao waliomba serikali iruhusu wauze kuku kwa kilo kuanzia shambani.

Waziri Ndaki alisema upangaji wa bei kwa macho bado uko katika minada mingi ya mazao ya nyama na kueleza kuwa ili kuondokana na tatizo hilo, wameamua kila mnada unaojengwa lazima uwe na mzani.

"Tunatakiwa tutoke huko si kwa kuku peke yake hata mazao mengine. Hii ndiyo itatoa faida kwa mfugaji. Minada tutakayojenga itakuwa na mizani ili tuuze kwa kilo. Kuhusu ombi lenu kuanzia, sasa ruksa wafugaji wa kuku wa Dar es Salaam na Pwani kuuza kuku kwa kilo, bei iamliwe na soko," alisema.

Kuhusu ombi la wafugaji la serikali kuwaondoa madalali wa kuku eneo la TAZARA jijini Dar es Salaam ambao wamekuwa wakiuza vifaranga kwa bei juu na wengine wasio na viwango, Waziri aliwaagiza watendaji walishughulikie ikiwezekana wafikishwe kwenye vyombo vya dola.

Pia waziri aliwataka watendaji wake waache kujifungia ofisini badala yake waende mtaani kufuatilia wale wanaofanya biashara ya ututoleshaji vifaranga bila kusajiliwa kwa sababu wamekuwa wakisababisha hasara kwa wafugaji kwa kuwauzia visivyo na ubora.

Kwa upande wa ubora wa chakula cha kuku, aliwataka wataalamu badala ya kusubiri kuletewa kwenye maabara ili wapime ubora, waende mtaani kukagua.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kuku wa Nyama (TABROFA), Costa Mrema, aliainisha mambo sita wanayoomba serikali iyafanyie kazi. Aliyataja mambo hayo kuwa ni kuwapo kwa machinjio ya kuku, kupandishwa bei ya vifaranga muda mfupi kwa kampuni zinazototolesha na kulazimishwa kununua chakula na kampuni za uuzaji kuku.

Naye Mkuu wa Maendeleo ya Biashara kutoka kampuni ya AKM Glitters, John Baitani, alitaja matatizo mengine kuwa ni kodi na tozo mbalimbali zinazofikia 42 wakati wa uingizaji nchini mitambo inayohusiana na ufugaji kuku.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kushoto), akifungua mkutano wa wadau wa kuku wa nyama, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichalwe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Madini yaingiza bilioni 2.9 Simiyu

**Na Happy Severine,** BARIADI

SEKTA ya madini mkoani Simiyu imeingiza Sh. bilioni 2 .9 kati ya Julai, 2020 na Januari, mwaka huu, sawa na asilimia 1,173 ya lengo lililowekwa na serikali.

Ofisa Madini Mkoa wa Shinyanga na Simiyu, Joseph Kumburu, alisema hayo jana katika mkutano na wachimbaji wadogo mkoani hapa uliofanyika kata ya Dutwa wilayani Bariadi.

"Mfano mwezi huu haujaisha, lakini tumekusanya Sh. milioni 430. Kwa hiyo mwezi ukiisha tutakuwa na zaidi ya Sh. bilioni tatu. Tumejiwekea makisio ya kila mwezi kukusanya Sh. milioni 600 hadi 700 tunakaribiana na Shinyanga ambayo ni kubwa," alisema Kumburu.

Mwenyekiti Chama cha Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Simiyu (SIMIREMA), Paul Matendele, alisema wataendelea kushughulikia matatizo ya wachimbaji hao kwa mujibu wa miongozo ya serikali.

"Kumekuwapo na wachimbaji wadogo wanapeleka matatizo yao tofauti na kwetu, kinyume na miongozo. Niwaombe sana kupitia semina hii mjifunze miongozo ya madini ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima," alisema Matendele.

Pia alisema baadhi ya wachimbaji wadogo wa madini wamekuwa wanachangia migogoro kwa kutokuheshimu chama cha wachimbaji wa madini.

Aliomba Wizara ya Madini kuendelea kutoa leseni za uchimbaji na kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo na kwamba wanunuzi wa madini waendelee kushirikiana na chama hicho.

**Baadhi ya wachimbaji wadogo wa madini wamekuwa wanachangia migogoro kwa kutokuheshimu chama cha wachimbaji wa madini.**

# Waondolewa hofu madai ya benki kuuzwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWENYEKITI wa Bodi ya Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL), Dk. Gervas Machimu, amewaondoa hofu wanachama wa ushirika na wateja kuwa benki hiyo haijauzwa kwa CRDB bali wamewekeza ndani ya benki hiyo kimkakati.

Dk. Machimu alisema hayo jana mbele ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alipofanya ziara katika benki hiyo mjini hapa na kuzungumza na baadhi ya wafanyakazi huku akisisitiza kuwa benki hiyo iko imara.

"Benki kwa sasa iko imara na wewe umeona mwenyewe katika kipindi cha miezi mitatu tumetoka hasara (upotevu) Sh. milioni 345 mpaka Sh. milioni 45. Hii inaonyesha wazi kuwa kazi kubwa imefanyika hasa katika kuboresha misingi ya usalama ndani ya benki na kukuza mtaji," alisema.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa benki hiyo ni kusaidia kuwainua wanaushirika kiuchumi na kudai kuwa tetesi zinazoenea mtaani kuhusu kuuzwa kwa benki hiyo kwa CRDB si za kweli.

Dk. Machimu alisema awali benki hiyo ilikuwa ikipitia katika matatizo, lakini kwa sasa imesimama imara na inaendelea kusimamia shughuli za kibenki na kubainisha kuwa mpaka sasa, hisa asilimia 14 zimeshauzwa na kwamba bado kuna fursa ya uwekezaji ndani ya benki hiyo.

"Japo tunaendelea kutoa huduma, tuna mambo tiunayokuomba Katibu Mkuu utusaidie ikiwamo kusukuma mashauri ya watu walioifanyia ubadhirifu benki yetu ambayo yako mahakamani pamoja na kutusaidia kupata Sh. bilioni tatu ambazo zilifanyiwa ubadhirifu," alisema Dk. Machimu.

Mwenyekiti huyo pia alimwomba Katibu Mkuu kuwasaidia kukamatwa watu walioihujumu benki hiyo ambao mpaka sasa bado hawajakamatwa akiwamo aliyekuwa ofisa mikopo wa benki.

Naye Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndege, aliwataka watumishi wa benki hiyo kuendelea kuwa wabunifu, kuongeza ufanisi kazini na kuwa tayari kupokea matatizo na kuyafanyia kazi.

Kusaya kwa upande wake aliwataka wafanyakazi wa benki hiyo kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu mkubwa ili kurejesha imani kwa wanaushirika.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa benki hiyo ni kuhakikisha inamkomboa mwanaushirika na kuwataka kufanya benki hiyo ifahamike ndani na nje ya nchi kwa kuitangaza.

"Niwatake mhakikishe ndani ya muda mfupi muwe na matawi mengi ndani ya nchi ili wateja wenu popote watakapokuwa wapate huduma. Pia hakikisheni panapokuwa na shughuli za ushirika ndani ya nchi hii, mnaenda kuitangaza benki," alisema.

Katibu Mkuu pia aliagiza wale wote ambao walikuwa wateja wa benki hiyo na wanadaiwa kuhakikisha wanalipa madeni haraka na wale wote watakaokaidi, watachukuliwa hatua za kisheria.

# Kaya 1,200 zaondolewa ruzuku TASAF

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WALENGWA 1,252 wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameondolewa kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini baada ya kukosa sifa.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Msalala wilayani hapa, Denis Pius, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kuzitembelea kaya za walengwa wa mfuko huo kwa lengo la kuona maendeleo yao katika kujikwamua kiuchumi.

Alibainisha katika halmashauri hiyo mwaka 2015 wakati walipoanza kutoa fedha za TASAF, kulikuwa na walengwa 4,805, lakini baada ya uhakiki mpya, wakabaki 3,553.

"Katika Halmashauri hii ya Msalala wilayani Kahama, tulifanya uhakiki upya wa walengwa wa TASAF na kuondoa kaya 1,252 baada ya kukosa sifa.

"Sifa hizo ni pamoja na walengwa kufariki dunia, wengine kuhama na baadhi kutokuwa na sifa za kuwa kwenye mpango huo," alisema Pius.

Alisema kuwa tangu halmashauri hiyo ianze kutoa fedha za ruzuku kwa walengwa wa TASAF mwaka 2015, kiasi cha Sh. bilioni 5.6 kimetumika.

Mmoja wa walengwa wa TASAF kutoka Kijiji cha Kisuke wilayani hapa, Ester Jilala, alisema fedha hizo zimekuwa mkombozi mkubwa katika maisha yake kumwinua kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Alisema fedha za TASAF zimemsaidia kujenga nyumba mbili za bati na kumsomesha mtoto wake hadi Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mnufaika huyo wa mfuko huo alibainisha kuwa sasa mwanawe huyo ni mwalimu wa sekondari mkoani Morogoro na hajamsahau mzazi wake katika kumsaidia fedha kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

**Fedha za TASAF zimemsaidia kujenga nyumba mbili za bati na kumsomesha mtoto wake hadi Chuo Kikuu cha Dodoma.**

# Washtakiwa dawa za kulevya watiwa hatiani, waachia huru

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, imewatia hatiani na kuwaachia huru washtakiwa wawili, Mkami Shirima na Emiliana Laizer, waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya usafirishaji na uuzaji wa dawa za kulevya aina ya mirungi.

Mkami Shirima ambaye ni mshtakiwa wa pili katika kesi hiyo ya kukutwa na kilogramu 2.95 za mirungi, bado anakabiliwa na kesi nyingine ya mauaji ya mfanyakazi wake wa ndani (house girl), Salome Zakaria.

Akisoma hukumu iliyowaachia huru washtakiwa hao, Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Gwantwa Mwankuga alidai kuwa vielelezo vya ushahidi vilivyotolewa na upande wa mashtaka katika kesi hiyo vilikuwa na mkanganyiko ambao mahakama imeshindwa kuwatia washtakiwa hatiani.

Hakimu Mwankuga, alidai kuwa kutokana na ushahidi huo kuwa na mkanganyiko, Mahakama hiyo imejiridhisha kuwa washtakiwa hawana hatia na inawaachia huru.

Washtakiwa wote kwa pamoja walidaiwa kutenda kosa hilo Septemba 24, mwaka 2019, katika eneo la Mianzini mkoani Arusha.

Kabla ya kukamatwa kwao, washtakiwa hao wanadaiwa kukutwa wakijaribu kufanya jaribio la kusafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi kilogram 2.9.

Baada ya Mahakama kuwaachia huru, Mkami Shirima aliendelea kuwa chini ya ulinzi wa polisi kutokana na kesi nyingine inayomkabili ya mauaji ya mfanyakazi wake wa ndani.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Baobab ya Mapinga Bagamoyo, wakishangaa sanamu ya mjusi mkubwa, walipofanya ziara ya mafunzo katika Makumbusho ya Taifa, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, chini ya ufadhili wa kampuni tanzu ya Global Education Link ya GEL Holiday Tours. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mamia wamuaga Vedasto Msungu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, jana aliongoza waandishi wa habari na wakazi wa Morogoro kuuaga mwili wa aliyekuwa mwandishi wa habari wa kituo cha ITV na Radio One, Vedasto Msungu.

Akizunguza katika ibada maalum iliyofanyika jana katika viwanja vya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Msulwa alisema alimtambua Msungu kama mwandishi mahiri wa habari aliyekuwa akitekeleza majukumu kwa weledi.

Alisema wakati wa uhai wake, Msungu alijitengenezea vyanzo vingi vya habari na kumfanya kutambulika ndani na nje ya nchi, hivyo kuwataka waandishi wa habari kufuata nyayo zake katika kukuza tasnia ya habari nchini.

"Ninafahamu Msungu tangu tukiwa wote katika kazi ya uandishi kwa zaidi ya miaka 20 sasa. Tofauti yetu ni kwamba alitengeneza wigo mpana wa vyanzo vya bahari pengine kushinda waandishi wengi wa wakati ule na hata sasa ndiyo maana tumeshuhudia akiripoti habari za kila sehemu ya nchi," alisema Msulwa.

Akitoa salamu za IPP Media, mwandishi wa ITV/Radio One mkoani Morogoro, Idda Mushi, alisema kuondokewa na Msungu ni pigo kubwa kwa familia ya IPP Media kwa sababu ni miongoni wa waandishi waandamizi ambao wameifanya ITV kuwa kinara wa upashaji wa habari katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mushi alisema enzi ya uhai wake, Msungu aliandika na kuripoti habari za aina mbalimbali hususani za uhifadhi, utalii na mazingira ambazo zilimpatia umaarufu mkubwa na kuongeza thamani ya habari zilizokuwa zinarushwa na kituo chake.

"Hili ni pigo kubwa kwetu na kwa taifa kwa ujumla kwa sababu ndugu yetu alikuwa mwanahabari mwandamizi na miongoni wa waandishi wa mwanzo kabisa wa ITV na Radio One. Kazi zake pia zimechangia kwa kiasi kikubwa taasisi hii kuwa bora Afrika Mashariki na Kati na kujipatia tuzo mbalimbali," alisema.

Baada ya ibada hiyo, mwili wa marehemu ulisafirishwa kwenda Uleling'ombe wilayani Kilosa kwa ajili ya mazishi yaitakayofanyika leo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF isilale kwa waamuzi lala salama Ligi Kuu Bara

**LIGI** Kuu Tanzania Bara ipo hatua ya lala salama ambapo leo inaingia raundi ya 21, huku Klabu ya Yanga ikiwa kileleni mwa msimamo baada ya kujikusanyia pointi 46 ikifuatiwa na Simba yenye alama 42, lakini ikiwa michezo miwili nyuma.

Mkiani mwa ligi hiyo ipo Mwadui FC ikiwa na pointi 15 sawa na Mbeya City inayofuatia katika nafasi ya pili kutoka mkiani baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 20 katika ligi hiyo inayoshirikisha jumla ya timu 18 msimu huu.

Msimu huu ligi imezidi kuwa ngumu na imeongeza mvuto jambo ambalo limeifanya kushika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika kwa mujibu wa viwango vya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), hivyo hilo ni jambo la kujivuni si tu kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), bali pia kwa wadau wote wa soka na Watanzania kwa ujumla.

Pamoja na kuwapo kwa changamoto nyingi, ikiwamo ubovu wa viwanja hususan kwa eneo la kuchezea 'pitch', lakini TFF na TPLB kuna haja ya kuwamulika waamuzi ili haki itendeke na si tu itendeke bali ionekane ikitendeka kweli kwa timu zote 18 zinazoshiriki ligi hiyo.

Tunafahamu tayari ligi hiyo imegawanyika katika makundi matatu makubwa, mosi ni kundi la timu zilizopo katika mbio za kuwania ubingwa ambazo ni Simba, Yanga na Azam FC, huku pakiwamo na timu zinazowania tu kuendelea kuwamo Ligi Kuu msimu ujao na zile zinazopigania kuepuka kushuka daraja.

Hivyo, pasipo waamuzi kuchezesha soka kwa kufuata sheria 17 za soka duniani kwa kuhakikisha haki inatendeka, tutashuhudia bingwa atakayepatikana akikosa sifa ya kuwa mwakilishi bora wa nchi katika michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika.

Lakini haki ikikosekana zitashuka daraja timu ambazo hazikustahili huku zitakazosalia Ligi Kuu zikiwa ni zile ambazo haziwezi kutoa changamoto na ushindani mkubwa hivyo kuiporomosha viwango ligi yetu ambayo imefika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika.

Lengo letu ni kuona Ligi Kuu Tanzania Bara ikizidi kupanda viwango hadi kufikia nafasi tatu za juu, na hilo litawezekana tu endapo changamoto zinazoikabili hususan ubovu wa viwanja zitashughulikiwa lakini waamuzi wakiongeza umakini na kuchezesha kwa haki kwa kufuata sheria 17 za soka duniani.

Presha imekuwa kubwa sana kwa waamuzi kutokana na katika baadhi ya michezo kushindwa kutafsiri vema sheria 17 za soka, jambo ambalo linawafanya mashabiki kuamini zipo timu zinabebwa ama waamuzi wanapenzi nazo.

Nipashe tunatambua yapo baadhi ya makosa yanayofanywa na waamuzi ambayo ni ya kibinadamu, lakini tunawataka kuongeza umakini zaidi kwa kuyapunguza ili kuifanya ligi yetu kupiga hatua kutoka hapo ilipo kwa kupanda ubora kwa kuwa moja kati ya ligi tatu bora barani Afrika.

Kwa mantiki hiyo, TFF na TPLB wanapaswa kuendelea kushughulikia changamoto zote hususan kutowafumbia macho waamuzi ambao wanashindwa kuchezesha kwa kufuata sheria 17 za soka ama kwa kurubuniwa na baadhi ya klabu au kwa mapenzi yao binafsi, ili kuulinda ubora wa ligi yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tamu tulikula sote...

Na Barnabas Maro

**"TAMU** tulikula sote na uchungu vumilia." Maana yake tulishirikiana wakati wa raha sasa yapasa kuuvumilia uchungu au kuyakabili matatizo.

Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu anayetamani kumkimbia mwenzake kwa kuwa kuna matatizo fulani yaliyozuka ingawa wakati wa raha walikuwa chanda na pete.

Kwa wale wasiomfahamu au waliomsahau mtu aitwae Jela Mtagwa, basi ni aliyekuwa mchezaji maarufu wa Yanga na timu ya Taifa (Taifa Stars) kwa muda mrefu kabla ya kustaafu. Kwa umahiri wake, Shirika la Posta na Simu ambalo liliweka picha ya sura yake kwenye moja ya stempu zake zilizotumiwa kutuma barua.

Ni mchezaji pekee wa Tanzania ambaye sura yake ilitumiwa na Shirika la Posta na Simu kati ya stempu zilizotumiwa na shirika hilo, ndani na nje ya nchi. Ni heshima aliyopewa Mtagwa, aliyekuwa mchezaji wa Yanga. Pamoja na ukweli huo, leo si timu ya Yanga wala ya Taifa inayomkumbuka mchezaji huyo ambaye sasa ni mgonjwa asiyekuwa na msaada wowote!

Mtagwa amekuwa mgonjwa kwa muda mrefu bila kupewa msaada wowote muhimu na timu yake ya Yanga wala Taifa (kwa maana ya TFF) wala Shirika la Posta na Simu lililovutiwa na uchezaji wake hata kutumia picha yake kwenye moja ya stempu zake.

Ni heshima ambayo hakuna mchezaji mwingine wa Tanzania aliyepewa heshima hiyo.

Kuna watu mbalimbali wanaokwenda kumjulia hali nyumbani kwake Magomeni jijini Dar es Salaam, lakini timu alizozitumikia mpaka alipostaafu, nazo "zimestaafu!" Kumsaidia!

Wiki iliyopita familia ya Mtagwa ilitoa kilio chake ikiomba msaada kwa wananchi kumsaidia mchezaji huyo asiyesahaulika! Wakati ule wachezaji hawakuwa wakilipwa mishahara kama ilivyo sasa bali ni 'asante' yaani fedha kiduchu zisizokidhi haja. Sasa wanalipwa mamilioni ya hela na kununuliwa magari ya kutembelea mitaani.

Je, wachezaji wa zamani hawana umoja, yaani chama chao cha kuwatetea na kuwasaidia mmoja wao apatapo shida?

Naomba nimwambie Mtagwa kuwa, " Mema na mabaya (maovu) ndio ulimwengu." Maana yake ulimwengu huwa na mambo mema na mabaya. Maneno haya hutumiwa kutukumbusha kwamba ulimwengu umejaa mema na maovu hivyo, tunapaswa kuyavumilia maovu au mabaya yatupatapo.

Jambo lingine linalokera ni baadhi ya waamuzi wetu wa kandanda na wasaidizi wao kama kweli husimamia haki wakati wanapochezesha viwanjani! Makosa ya wazi yanayofanywa viwanjani yanakuwa na shaka yaani hali ya mtu kuwa na wasiwasi juu ya jambo miongoni mwa watazamaji.

Wakati mwingine waamuzi hutoa adhabu zilizo kinyume kabisa na vitendo vinavyotendeka viwanjani! Mchezaji aweza kufanyiwa rafu ya wazi lakini mwamuzi na wasaidizi wake wasione tukio hilo au kutoa adhabu upande uliofanyiwa rafu! Pia hutoa uamuzi wa kushangaza pale mchezaji wa upande mmoja chama kuunawa mpira eneo la goli lakini asitoe adhabu ya penalti au kuruhusu penalti yenye utata!

Huwa najiuliza: Hufanya hivyo kwa kuwa anaishabikia moja ya timu iliyo uwanjani au hupewa rushwa na timu anayoipendelea.?

Hali hii inapokuwa hivyo Chama cha Waamuzi, au TFF huwachukulia hatua gani au viongozi wa TFF nao wamegawanyika katika kuzipenda Yanga na Simba? Kwa kushindwa kufuata kanuni na sheria ndogondogo zilizoundwa kurahisisha utekelezaji wa sheria mama inayosimamia jambo fulani?

Yapo mambo mengi yanayofanywa na wachezaji viwanjani, lakini hakuna hatua mujarabu zichukuliwazo dhidi yao. Mfano, mpira unatoka nje ya uwanja lakini mrushaji anarusha hatua sita au saba kutoka eneo uliotokea. Waamuzi na wasaidizi wao huwa kimya!

Kama hiyo haitoshi, baadhi ya wachezaji wanapoonywa huwadharau waamuzi kwa kuwarushia mikono kuonesha dharau dhidi yao! Hata kama wana malalamiko ya haki, hawapaswi kuwadharau waamuzi.

Ilivyo siku hizi waamuzi wanadharauliwa sana na wachezaji wasiokuwa na adabu yaani utaratibu unaokubalika katika kufanya jambo; heshima, nidhamu.

Ni wajibu wa klabu za kandanda kuwafunza wachezaji wao taratibu zote wanazopaswa kufuata wanapokuwa viwanjani, viongozi wao wanapowaonya haifai kuwabeza na kuonesha dharau. Je, wao (watakubali kudharauliwa mbele ya halaiki (idadi kubwa ya mkusanyiko wa watu?), tafakari.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784844096***

# KWAHERI BALOZI MHANDISI JOHN WILLIAM KIJAZI




Rais Dk. John Magufuli akizungumza wakati wa kutoa heshima za mwisho kwa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Balozi John William Kijazi. Waliokaa (kutoka kushoto) ni Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma na Naibu Spika Dk. Tulia Ackson. **PICHA: IKULU**




Katibu Mkuu Ikulu, Dk. Moses Kusiluka na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Uwekezaji), Dorothy Mwaluko, wakiwa wamebeba shada la maua lenye herusi KMK yaani Katibu Mkuu Kiongozi, wakati wa kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Kijazi. **PICHA: IKULU**



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na kuifariji familia ya marehemu Mhandisi Balozi John William Kijazi, baada ya kumalizika kwa ibada na misa maalum kwa ajili ya kumwombea. **PICHA: OMR**




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiaga mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Balozi John William Kijazi. **PICHA: OMR**



Jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Balozi John William Kijazi, likiwa katika Viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya ibada na hafla ya kuuga. **PICHA: OMR**



Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali wakiwa katika foleni ya kumuaga Balozi Mhandisi John Kijazi. **PICHA: IKULU**

# Wachanga fedha kujenga zahanati

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

WAKAZI wa Kijiji cha Jengeni, Kalambo mkoani Rukwa, wameanza kuchangishana Sh. 10,000 kila kaya kwa lengo la kujenga zahanati ya kijiji kutokana na kile walichodai wamechoka kutembea kilomita 15 kufuata huduma za afya.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakazi hao walisema wamelazimika kufanya hivyo kutokana na kijiji chao kutokuwa na zahanati, kitendo kinachosababisha usumbufu mkubwa kwa wajawazito na watoto.

Mmoja wa wananchi hao, Leonard Sichone, alisema wameweka lengo la kuchangia fedha hizo na kwamba kutokana na hali ya uchumi, kila kaya itachangia kwa awamu mbili ya Sh. 5,000 kila moja.

Mkazi mwingine, Francis Sichula, alisema wamejiwekea lengo kufikia Juni, mwaka huu, kuanza kuchimba msingi na sasa wako katika hatua ya kusomba mawe na kupeleka katika eneo la ujenzi.

Mmoja wa wanawake wa kijiji hicho, Flaviana Siyame, alisema wanakabiliwa na wakati mgumu pindi wanapokuwa wajawazito au kuwapeleka watoto kliniki kwa kuwa wanalazimika kutembea kilomita 15 kufuata huduma za afya katika kijiji cha jirani cha Kaluko.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kalambo, Emily Mwakajinga, alisema changamoto hiyo wanaifahamu na katika bajeti ya mwaka 2021/22, halmashauri imetenga Sh. bilioni 11.589 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.Alisema fedha hizo pia zitatumika kujenga na kukarabati miundombinu ya afya ikiwamo ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Katete ili kuwaondolea adha wananchi hao.




Meneja wa Bidhaa za Tigo, Mkumbo Muyonga, akizungumza wakati wa uzinduzi wa simu mpya ya Infinix Hot 10 play, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa Infinix, Aisha Karupa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC azitaka DAWASA, TANESCO kubadilika

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amezitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuachana na mipango ya kwenye makaratasi na badala yake kufanya uhalisia kwa kupeleka huduma kwa wananchi.

Ndikilo alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea kituo cha kupoozea umeme cha Mlandizi kujionea namna TANESCO mkoa wa Pwani ilivyojipanga kuboresha usambazaji wa umeme.

"DAWASA tunaomba waache mipango ya kwenye karatasi. Pelekeni maji Zegereni eneo la viwanda, kuna viwanda 25 vyote vinahitaji huduma. Kiko kiwanda cha dawa za binadamu kikikamilika kitasaidia kuokoa fedha kwa kuagiza dawa nje ya nchi na mtaa wa Zogowale kuna wananchi wana uhitaji," alisema Ndikilo.

Alisema kila taasisi wezeshi inatakiwa kusimamia mipango waliyokubaliana katika kikao na mkuu wa mkoa namna ya kufikisha huduma kwenye maeneo ya viwanda na wananchi.

Mkuu huyo wa mkoa alitoa wito kwa shirika hilo kuendelea kusambaza umeme kwa wananchi ili wafanye shughuli nyingine za kimaendeleo.

Ndikilo pia aliwataka wananchi na wamiliki wa viwanda kulipa bili kwa wakati ili fedha zinazopatikana zitumike kuendelea kufanyia maboresho katika nishati ya umeme.

Mkuu wa Mkoa alimpongeza meneja wa TANESCO Mkoa wa Pwani, Mhandisi Mahwa Mkaka, kwa jitihada anazofanya kufanikisha wananchi na wawekezaji wa viwandani wanapata umeme wa kutosha.

Naye Mkaka alisema hadi sasa wana wateja 180,000 na kwamba mahitaji katika mkoa huo ni megawati 117.8 na ifikapo Machi 4, wanatarajia kuwasha transfoma ya MVA 120 itakayoondoa tatizo la umeme viwandani.

Mkaka amewataka wawekezaji kufika kuwekeza katika mkoa huo kwa kuwa upo umeme wa uhakika na kwamba upo mradi wa MVA 240 ambao utamaliza tatizo la umeme hususani maeneo ambayo bado yatakuwa na tatizo.

Pia alisema iko miradi ya ujazilizi na maeneo 116 yamepata umeme na TANESCO na maeneo 121 ambayo yanaendelea kusambaziwa umeme na kufanya ukarabati kwenye miundombinu ya nishati hiyo.

# Wazalishaji mabati wapewa elimu viwango

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA ya Viwango Tanzania (TBS) limetoa mafunzo kwa wazalishaji, waagizaji, wasambazaji na wadau mbalimbali wa mabati nchini ili kuwezesha kuzalisha na kusambaza mabati yenye viwango vinavyotakiwa.

Mafunzo haya yameandaliwa baada ya Tanzania kukamilisha utaratibu wa kupitisha viwango vya mabati.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati akifungua mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, David Ndibalema, alisema mafunzo hayo yanalenga kutilia mkazo usimamiaji wa viwango.

Alisema lengo ni kudhibiti ubora na kuhakikisha biashara hiyo inafanyika katika mfumo unaoeleweka na kukubalika kisheria sambamba na kanuni zinazosimamia mifumo viwango na udhibiti ubora.

Ndibalema alisema watumiaji wa bidhaa hizo mara nyingi hutegemea wasambazaji wanaosambaza bidhaa zenye ubora kwa ajili ya kuezekea nyumba zao.

"Ikiwa mtumiaji hawezi kupata mabati yenye ubora na yanayoendana na mahitaji yake hii inasababisha kuwapo kwa malalamiko," alisema.

TBS, alisema ilifanya tathmini na kubaini kuwapo mabati na koili zinazozalishwa na kuingizwa nchini bila kukidhi matakwa ya viwango.

"Baada ya kuona bidhaa za mabati zinazalishwa na kuingia nchini zikiwa hazina viwango vya ubora tukaona tuitishe mafunzo haya ili tuyatumia kuweka mikakati ya kutatua changamoto hizo," alisema.

Ndibalema alisema katika mafunzo hayo, kutakuwa na wawezeshaji kutoka TBS ambao watatoa mada kuhusu viwango na matakwa ya viwango vya mabati vilivyowianishwa katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupitishwa kuwa viwango vya kitaifa.

Pia alisema kutakuwapo na mada zingine za udhibiti ubora na changamoto za mabati yaliyopo sokoni.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Uandaaji Viwango wa TBS, Henry Massawe, alisema viwango vinaandaliwa na wadau kupitia kamati zao za kitaalamu pamoja na mfumo wa jumla wa utoaji maoni ya wadau.

Alisema mafunzo hayo ni sehemu mojawapo ya utaratibu mchakato wa kuandaa viwango, hivyo wamekutana na wadau kujadili viwango hivyo ili kuwajengea uelewa katika suala zima la viwango.

Pia alisema kukutanisha wadau hao ni kuwapa uelewa wa pamoja wa kiwango cha kitaifa katika kurahisisha utekelezaji wake na kufanya biashara kwa urahisi hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki.



# Wanaofanya kazi wanazoweza wazawa sasa watumiwa salamu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, amesema serikali haitasita kumwondoa raia wa kigeni atakayebainika kufanya kazi ambayo Mtanzania ana utaalamu wa kuifanya ili kulinda ajira za wazawa.

Aidha, amewataka vijana kuacha kuchagua kazi kwa kuwa serikali imeweka mazingira mazuri ya kujiajiri.

Katambi alisema hayo jana alipokuwa akizindua duka la dawa la Ngumo lililoko mtaa wa Chang'ombe jijini hapa ambalo limeanzishwa na vijana wawili wahitimu wa vyuo vikuu katika ngazi mbalimbali. Alisema dhamira ya serikali si kumwonea mtu bali ni kulinda ajira za wazawa.

Akizungumzia ajira kwa vijana, Katambi aliwataka wahitimu wa vyuo nchini kuacha kubweteka kusubiri ajira serikalini kwa kuwa ziko fursa mbalimbali za kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Vijana, kwa mujibu wa Katambi, wamekuwa akilalamika kwamba hakuna ajira bila kutumia fursa zilizopo ikiwamo mikopo inayotolewa na halmashauri nchini.

"Tumekuwa tukilalamika kuwa hakuna ajira wakati miradi mikubwa ya maendeleo kwa mfano wa uzalishaji umeme bwawa la Mwalimu Nyerere peke yake limeajiri watu 60,000 na asilimia 65 ni vijana," alisema.

**Vijana wanatufundisha ukiwaza vizuri kwenye nia yako itakusaidia kupata rasilimali za kufanikiwa, wameanza na wanataka kuingia kwenye soko la dunia la uuzaji wa dawa.**

Katambi alisema miradi yote ya maendeleo vijana wamepewa nafasi kubwa ya ajira kwa asilimia 85 huku akisema kuna tatizo la vijana wanawaza mambo makubwa.

"Tatizo sisi vijana tunawaza makubwa. Mtu anawaza akiajiriwa apate mshahara mkubwa na gari na vijana tukiingia tu ofisi tunawaza kupiga dili," alisema huku akiwataka kuwa na malengo na wanapokopeshwa fedha warudishe kwa uaminifu.

"Chuo Kikuu serikali inatoa fedha za mikopo na uwekezaji kwenye sekta ya elimu ni mkubwa sana. Zaidi ya Sh. bilioni 300 zinatolewa, ni aibu kwa kijana kukaa nyumbani kusema hujaajiriwa," alisema.

"Vijana wanatufundisha ukiwaza vizuri kwenye nia yako itakusaidia kupata rasilimali za kufanikiwa, wameanza na wanataka kuingia kwenye soko la dunia la uuzaji wa dawa," aliongeza.

Alitoa rai kwa vijana hao waliofungua duka la dawa kusimamia weledi, elimu na taaluma katika kufanya kazi hiyo ili kuwa na ubora wa huduma na biashara.

"Mchawi wa biashara wa kwanza ni kauli yako kwa mteja. Utoaji wa huduma kwa mteja, usafi tunauza dawa zinazogusa maisha ya binadamu," alisema huku akiwataka kuwa waaminifu na kuondokana na uchakachuaji wa dawa na kuuza dawa zilizoisha muda.

"Muwe waaminifu katika kuuza dawa, msichakachue, na usiuze dawa kama una mashaka nayo, usiweke mbele fedha kuliko utu, nawahakikishia mtaenda mbali zaidi ya hapa," alisema.

Alisisitiza kutumia taaluma zao vizuri na kutopandisha bei isivyostahili kwa kuumiza wananchi.

"Usipate manufaa ya kujinufaisha kupitia ugonjwa wa mtu, msishiriki katika mambo ya utoaji mimba na uchomaji mimba, muyaepuke hayo, ili kuepuka mkono wa dola," alisema.

Katambi alikemea uuzaji wa dawa zinazoleta madhara kwa binadamu ikiwamo za usingizi.

Naye Ofisa Uendeshaji wa duka hilo, Selemani Kisongo, alisema duka hilo limeanzishwa na vijana ambao ni wahitimu wa chuo ngazi mbalimbali.

"Dhamira yetu ni kuboresha huduma ya afya kwa wananchi na kutoa huduma kwa kiwango cha juu, kuwa wabunifu, kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni, kuzingatia miiko ya uendeshaji maduka ya dawa na vipodozi," alisema.



Mbunge wa Mpwapwa, George Malima (kushoto), akizungumza na baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Makutupa, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma juzi, katika mkutano wake wa kuhamasisha miradi ya maendeleo jimboni humo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Vijiji tisa Bahi vyakosa umeme

**Na Mwandishi Wetu,** BAHI

VIJIJI tisa vya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma ambavyo bado havijaunganishwa na huduma ya umeme, viko mbioni kupatiwa nishati hiyo.

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Bahi, Brayson Kitila, aliyasema hayo jana katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani kujadili maendeleo na bajeti ya halmashauri.

Mhandisi Kitila alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha vijiji vyote vinapatiwa umeme.

"Kati ya vijiji 59 vilivyo na umeme ni 50 na bado vijiji tisa na kazi inaendelea kwenye Kata za Ilindi, Babayu, Zanka na makandarasi wako kazini," alisema.

Alisema kazi katika vijiji tisa inaendelea licha ya kuwapo na tatizo la wizi wa vifaa na juhudi za kuvisaka zinaendelea.

Kazi, alisema zinaendelea vizuri na katika vijiji vya Lukali, Kongongo na Zanka kazi imekamilika kwa asilimia 97 na ifikapo Februari 28, mwaka huu, vijiji vitatu vya Ilindi, Babayu na Zanka viwe vimepata nishati ya umeme.

"Vijiji vingine vilivyosalia vitapatiwa umeme mwaka huu na kazi itakayobaki ni kuanza kusambaza kwenye vitongoji kama serikali ilivyokusudia kusambaza umeme kwenye vijiji na vitongoji nchi nzima," alisema.

"Kuna kituo cha kusambaza umeme kinajengwa Mtera na kikikamilika kitaweza kusambaza umeme katika Wilaya za Mpwapwa, Kongwa na Bahi," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kuwa walinzi wa miundombinu ya umeme kwa kuacha kuchomba mashamba hali inayosababisha nguzo kuungua.

Alisema kuna matukio ya kuungua nguzo za umeme katika vijiji vya Lamaiti, Mwitikila na Mzogole.

Kwa upande mwingine, Diwani wa Bahi, Augustine Ndonu, alitaka juhudi kuelekezwa kwa wazalishaji wenye viwanda ili kuzalisha bidhaa zenye ubora ambapo eneo hilo lina viwanda zaidi ya saba.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Pius Mwaluko, alisema kuna haja kwa madiwani kukaa na wajasiriamali wadogo ili wapate elimu itakayoinua biashara zao.

# Utatuzi kero za madereva waanza rasmi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMISHNA wa Kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Brigedia Jenerali Francis Mbindi, ametoa siku saba kwa wadau kuwasilisha maoni yao kuhusu mpango kazi wa kutatua kero za madereva.

Aidha, amewataka wamiliki wa vyombo vya usafiri nchini kuwapa mikataba iliyoboreshwa ya ajira madereva ili kuipa hadhi inayostahili kazi hiyo na kuboresha huduma ya usafirishaji. Kamishna huyo alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumzia serikali inavyoshughulikia kero ya wafanyakazi katika sekta ya usafirishaji.

Alisema hatua hiyo ni kutokana na maazimio yaliyofikiwa katika kikao cha mashauriano na wamiliki, wadau wa usafirishaji na viongozi wa vyama vya wafanyakazi madereva kilichofanyika Desemba 19, mwaka jana.

Akizungumzia hatua ambayo serikali imekuwa ikichukuliwa kutatua kero za madereva, alisema hushirikiana wadau wa sekta ya usafiri na usafirishaji vikiwamo vyama vya wafanyakazi madereva na vyama vya wamiliki wa vyombo vya usafiri na usafirishaji hatua iliyowezesha kuundwa kwa kamati maalumu.

Jenerali Mbindi alisema uamuzi huo ni kutokana na ahadi ya Rais John Magufuli aliyoitoa Novemba 13, mwaka jana, wakati akizindua Bunge la 12 kuwa itahakikisha wamiliki wa magari wanatoa mikataba ya ajira kwa madereva ili sekta hiyo kuwa na tija.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi hiyo, Jenista Mhagama, aliagiza kusimamia mikataba ya ajira husan ya madereva na kwamba ofisi yake ilishakutana na wadau na kutengeneza mpango kazi.



# Serikali Z'bar yasitisha biashara ya mchanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji na Nishati, Suleiman Masoud Makame, amesema Zanzibar inakabiliwa na uhaba mkubwa wa mchanga na serikali imesitisha biashara hiyo kwa wafanyabiashara na kampuni kubwa za ujenzi.

Makame alisema hayo jana wakati akitoa taarifa na hali ya uhaba wa mchanga na kubainisha kuwa wizara imefungua shimo lingine kwa ajili ya kuchota mchanga huku kukiwa na udhibiti mkubwa.

**Kuanzia sasa hakuna watu wakaoruhusiwa kuhifadhi mchanga katika maeneo yao ikiwamo katika viwanda vya kufyatua matofali.**

Alisema kuanzia sasa wizara imeweka utaratibu mpya na kupitia utaratibu huo, watu wenye mahitaji makubwa ya mchanga zikiwamo taasisi zinazojishughulisha na miradi ya ujenzi wa nyumba watalazimika kuandika barua kwenda wizarani.

"Tunakabiliwa na uhaba mkubwa wa mchanga hivi sasa. Kuanzia sasa hakuna biashara ya mchanga itakayofanywa na wale wenye mahitaji makubwa ya rasilimali hiyo," alisema.

Pia alisema watu wenye mahitaji chini ya tani 30 watalazimika kujaza fomu na kupelekewa mchanga katika maeneo yao ya kazi.

Alisema kuanzia sasa hakuna watu wakaoruhusiwa kuhifadhi mchanga katika maeneo yao ikiwamo katika viwanda vya kufyatua matofali.

Uhaba wa mchanga na utaratibu mpya wa upatikanaji wake kwa kiasi kikubwa unasababisha kupanda kwa gharama za ujenzi ikiwemo bei ya matofali kupanda.

Eneo la asilimia 30 la ardhi ya Zanzibar ndilo linalopatikana mchanga kwa ajili ya shughuli za ujenzi, huku asilimia 60 ya visiwa vya Zanzibar katika maeneo ya kusini Unguja ni jiwe na kiwango kilichobaki ni udongo.



Mkurugenzi Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Zanzibar, Dk. Haji Salim Khamis, akizungumza na washiriki wa mafunzo ya siku tano ya kuwajengea uwezo mabwana shamba na mabibi shamba kuhusu utoaji wa huduma katika kilimo cha shamba darasa, mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ataja vipaumbele uchumi buluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema asilimia 80 ya vipaumbele vya kitaifa kwa mwaka 2021-22 vitajikita katika kuimarisha miundombinu ya uchumi na uwekezaji katika kuelekea uchumi wa buluu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, alisema hayo wakati akiwasilisha mwelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo na bajeti kwa mwaka 2021/22 na 2023/24.

Aliutaja mradi wa matayarisho wa ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi Mangapwani mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na Mpigaduri na mkoani Pemba.

Kassim alisema ujenzi wa miradi ya bandari ambayo itazishirikisha sekta binafsi ni muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi ikiwa ni moja ya hatua ya safari kuelekea uchumi wa buluu.

Alisema katika juhudi zinazochukuliwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kukifanya kisiwa cha Pemba kuwa maalumu kwa ajili ya miradi ya uwekezaji, ujenzi wa Bandari ya Mkoani kuwa lango kuu la kiuchumi kwa mikoa jirani ya Tanzania Bara hadi Mombasa ni muhimu.

"Katika mradi wa Bandari ya Mpigaduri pamoja na Mkoani Pemba, tayari tumefikiwa hatua muhimu ya kutia saini makubaliano ya awali kwa kushirikiana na wawekezaji mbalimbali wa kimataifa kufanya upembuzi," alisema.

Aidha, aliutaja mradi wa miundombinu wa ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya kilomita 22.1 ya Chakechake hadi Wete ambayo ni kiungo kizuri ya mikoa miwili ya Pemba.

Vipaumbele vingine vilivyotangazwa na Waziri Kassim ni pamoja na kuendeleza juhudi za ujenzi wa viwanda vidogo vya usanifu wa mazao ya baharini kama vile mwani, chumvi na samaki.

Alisema katika kufikia uchumi wa buluu, ni muhimu kuimarisha kilimo cha mazao ya baharini ikiwamo ufugaji wa samaki, kilimo cha mwani ambacho kimeonyesha mafanikio makubwa kwa kundi kubwa la wanawake.

# Wizara yakabidhiwa mradi ujenzi studio

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imekabidhi mradi wa ujenzi wa ofisi ya studio ya Mkanjuni Pemba kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Hamad Rajab, alisema ameupokea mradi huo kwa hatua ya awali.

Hata hivyo, alisema ataunda tume ya uchunguzi kuhakikisha fedha za mradi zimetumika kama alivyoelezwa ili kujiridhisha.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba fedha za serikali ambazo zinatolewa kwa ajili ya ujenzi miradi mbalimbali, zitumike ipasavyo kwa maslahi ya umma.

Serikali, alisema haitamfumbia macho yeyote atakayefanya ubadhirifu wa fedha zinazotokana na jasho la wanyonge na kuhakikisha inawachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kurejesha walizotumia kwa maslahi yao.

"Niseme tu nimepokea mradi wa ujenzi wa jengo hili ila nitaunda kamati itakayochunguza fedha zilizotajwa kutumika hapa zinaendana na thamani ya jengo hili na itakapobainika kuna ubadhirifu sitasita kuwachukulia hatua zinazostahiki," alisema katibu huyo.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Dk. Khamis Abdallah Said, aliushauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kushirikiana na wizara yake katika kuliingizia mapato taifa ikiwamo kupanua wigo wa huduma za utalii kupitia michezo na utamaduni.

Kuhusu ujenzi huo, Mhandisi Mkuu Ali Mbarouk Juma, alishauri kuongezewa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa uzio na kisima kutokana na ofisi hiyo kuwa sehemu nyeti na kuwa karibu na makazi ya watu.

Mkurugenzi Mipango wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Omar Hamad, alisema mradi huo unaojengwa na serikali ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni moja, unatarajiwa kumalizika Aprili, mwaka huu.

**Lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba fedha za serikali ambazo zinatolewa kwa ajili ya ujenzi miradi mbalimbali, zitumike ipasavyo kwa maslahi ya umma.**



## PROFESA JAY

UKURASA 13





# KATINDINGANYA!

# Paula kaharibu kila kitu, sasa joto hasira

KATINDINGANYA! Ni msemo maarufu kusini mwa Tanzania ambao una maana ya kuharibu, kuchanganya au kufikisha jambo mahali pasipofaa.

Ndivyo ilivyokuwa kwa mwanamuziki maarufu nchini Rayvanny na Paula ambaye ni mtoto wa mwigizaji Kajala Masanja, walivyofanya na kusababisha vurumai kubwa kutokea hadi kufikia hatua ya kupelekana polisi.

Hata hivyo, baadhi ya wafuatiliaji wa mastaa hao, wanasema suala la kuvuja kwa picha za Rayvanny na Paula, isingekuwa na tukio kubwa kama Kajala asingekuwa na uhusiano wa kimapenzi na Harmonize.

Wanadai hasira zinazoonekana sasa baada ya kusambaa kwa picha hizo katika mitandao ya kijamii, inatokana na kuharibu mipango mahususi ya Harmonize ya kuongeza umaarufu wake kutokana na uhusiano wake na mama wa binti huyo.

"Unajua suala la mapenzi ya Harmonize na Kajala lilitawala katika mitandao ya kijamii, ilikuwa kete muhimu kwa Harmonize kuongeza umaarufu wake, lakini ilikatishwa ghafla na kuibuka kwa picha Rayvanny na Paula na kugeuza upepo," anasema Saidi Msanjila.

Anasema Harmonize alifanikiwa kuwateka Watanzania na kumfuatilia kila hatua wakati akiwa Zanzibar na Kajala, kila siku alitoa picha na taarifa mpya zinazowahusu ambazo ziliwavutia watu.

Hata hivyo, mambo yaliharibika baada ya Rayvanny kuchapisha picha hizo na kusababisha watu kugeukia upande wa pili na kuacha kutazama filamu ya mastaa hao.

Kutokana na hali ilivyo sasa ni wazi uhusiano kati ya Kajala na Hamisa Mobeto umevurugika, huku Harmonize na Rayvanny wamenuniana.

Tayari polisi imetoa taarifa yake kuwa iliwashikilia na kuwachilia kwa dhamana Rayvanny na Hamisa, kwa kosa la kuchapisha picha pila ridhaa ya upande wa pili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni ACP Japhet Kibona, amekiri wasanii hao walikuwa wanashikiliwa polisi kituo cha Osterbay, kabla ya kuachiwa.

**"Ni kweli walikamatwa jana, hii ni kesi ya polisi na hupaswi kueleza walichokizungumza ni nini ila kilichopo ni kusambaza picha kwenye mtandao bila ridhaa ya mmoja wapo mwenye hizo picha, Hamisa na Rayvanny walidhaminiwa wote". Amesema.**

BASI SAWA

## Miss Bella ulikutana nao wapi vile?

MSANII wa Bongo Fleva, Miss Bella, amesema wapo wanaojitamba wameokoka lakini wanakutana katika kumbi za starehe kunywa pombe.

Akizungumza na EATV, Miss Bella amesema imani ya mtu hujengwa na yeye mwenyewe na sio kujinadi, kwani wapo wengi ambao wanajitangaza kumtumikia Mungu, lakini kila siku wanakutana katika sehemu ya vinywaji vikali.

"Imani yangu ya kidini itabaki moyoni mwangu siwezi kujitangaza kama wanavyofanya wengine, amini kuna baadhi wamesema wanarudi kwa Mungu, lakini tunakutaka kumbi za starehe tunakunywa pombe pamoja," amesema.



## Kalala Junior, Papii wakutana Tukuyu Sound

MWIMBAJI nyota wa muziki wa dansi, Kalala Junior, amesema yeye na mwenzake Papii Kocha, wameungana na kuanzisha bendi iitwayo Tukuyu Sound.

Amesema, bendi hiyo ina muda wa mwezi mmoja ikiendelea kujiimarisha katika soko la dansi kwa kuandaa nyimbo mpya.

"Historia yetu inafanana, kutokana na ukweli kwamba wote ni sisi ni watoto wa wanamuziki wakongwe, hivyo tumeona tuungane ili kuendeleza vipaji vya wazee wetu," amesema Kalala Junior.






## Harmonize miezi mitatu tu ilikushinda?

MWANAMUZIKI na mmiliki wa lebo ya Konde Gang Music, Harmonize amefunguka kuwa alichepuka kwa bahati mbaya wakati wa ndoa yake, kutokana na mkewe Sarah kuwa mbali kwa muda mrefu.

Amesema kutokana na umbali wa mapenzi kati yake na aliyekuwa mke wake, hakuweza kuvumilia na ilimfanya kuchepuka na mwanamke mwengine ambaye amezaa naye mtoto mmoja wa kike.

"Ishu za Sarah hazikunisumbua, sio kama nilikuwa simpendi, yeye alisafiri akakaa kama miezi mitatu kwa sababu alikuwa na matatizo ya kifamilia kwao, kwa hiyo nikajikutana na mwanamke mwingine," amesema.



## Profesa Jay siku nyingine utaua mtu

MWANA Hiphop na aliyekuwa Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule maarufu 'Profesa Jay' ametoboa siri kwamba aliwahi kumpeleka mchepuko nyumbani kwa mkewe Grace Mgonjo, wakati walipokuwa wamegombana.

Prof. Jay amesema mapenzi kati yake na mkewe huyo yamepitia mambo mengi, na kuelezea siku hiyo alipompeleka mchepuko alimuona mkewe huyo akitetemeka kama simu ya mkononi ikiita.

"Uhusiano wetu umepitia kushuka na kupanda hadi tukaachana, yeye akawa na mahusiano na mimi nikawa na mahusiano mengine, sasa kwa bahati mbaya nikambebea yule niliyekuwa naye kwenye mahusiano na nikaenda naye kwa mke wangu, kitu hicho kilimuumiza kuliko vitu vyake vingine, nilimuona akitetemeka kama simu," amesema Prof. Jay.

## WAPIGA GITAA MAHIRI KWA UTUNZI

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE muziki wa dansi mara nyingi watunzi wa nyimbo wanakuwa ni waimbaji. Karibuni asilimia 80 hadi 90 ya nyimbo nyingi za dansi zinatungwa na waimbaji.

Ndiyo maana utaona kama kina "Tx Moshi Wiliam, Selemani Mbwembwe, Muhidini Gurumo, Hassan Bitchuka, Fresh Jumbe, Shaaban Dede, Hemed Maneti, Jerry Nashon 'Dudumizi', Athumani Momba, wakivuma kwa tunzi nyingi nchini Tanzania.

Hata hivyo, kuna wanamuziki ambao ni wapiga vyombo ambao waliondokea kuwa maarufu sana kwa utunzi.

Na wengine wao ni wapiga magita ongozi, yaani solo. Leo tutawaangalia wapiga magita ambao walizibeba bendi zao kwa utunzi, wakitunga nyimbo kali na kuwaachia waimbaji wakifanya kazi yao, huku wenyewe wakiwa kwenye magitaa.

Katika kundi hili hatokuwapo Marijani Rajab kwa sababu kwa muda mrefu yeye alikuwa anaimba tu na alikuja kupiga solo muda mrefu baadaye, tofauti na wenzake ambao walianza moja kwa moja na magita na wakawa watunzi pia.

**Freddie Ndala Kasheba**

Alikuwa kiongozi wa bendi ya Orchestra Safari Sound (OSS), wakati ikitumia mtindo wa Dukuduku.


Kasheba ndiye aliyekuwa mtunzi wa nyimbo karibuni zote zilizoibeba bendi hiyo, lakini mwenyewe akipiga gitaa la solo. Tofauti na wengine, yeye alikuwa akapiga gitaa la nyuzi 12, ambalo watoto wa mjini wakati huo waliiita dazani, mwenyewe akiliiita kombora. Kwa kawaida gitaa la solo na rhythm lina nyuzi sita.

Nyimbo kama 'Takadiri', 'Mpakamanga', 'Ashura,', 'Dunia Msongamano', 'Gaba', na nyinginezo. Na hata alipoasisi kundi lake la Zaita Musica, alitunga kibao kilichotingisha sana kiitwacho 'Kesi ya Khanga.'

**Patrick Balisidya**

Balisidya ambaye aliliongoza kundi la Afro Band, ambalo umaarufu wake ulijulikana kama Afro 70, licha ya kupiga solo, lakini ndiye aliyekuwa mtunzi tegemeo kwenye bendi hiyo.

Mwanamuziki huyo ambaye ni marehemu, alitunga nyimbo nyingi zilizoifanya bendi hiyo kuwa maarufu sana ndani na nje ya nchi kama vile 'Dada Lida', 'Naomba Tusahauliane', 'Dirishani', 'Wekiendi', 'Wema Hawana Maisha', na nyingine nyingi.



**Nguza Mbangu Viking 'Babu Seya'**

Ikumbukwe kuwa mwanamuziki huyu alikuwa akiiongoza bendi ya Maquiz de Zaire na baadaye ikaitwa Maquiz Original.

Babu Seya alitunga karibia asilimia 80 ya nyimbo zote za bendi hiyo, mwenyewe akiwa haimbi, badala yake anawapa wengine wafanye kazi hiyo, yeye akikung'uta gitaa la solo.

Nyimbo maarufu ambazo alizitunga ni 'Seya', 'Ni Wewe Pekee', 'Sofia', 'Maida', 'Kiongo', na nyingine nyingi.

**Joseph Mulenga**

Alikuwa mpiga solo wa bendi mbalimbali, lakini bendi iliyomtangaza zaidi ni DDC Mlimani Park Orchestra.

Mulenga ambaye alikuwa akipiga solo, alitunga nyimbo nyingi zilizokuwa maarufu, zikiimbwa na kila Bitchuka na Gurumo kama vile 'Uhuru wa Zimbabwe', 'Pata Potea', 'Talaka ya Hasira', na nyinginezo.

**Hamza Kalala**

Achilia mbali kuwa ni mtunzi wa nyimbo zote kwenye bendi yote ya Bantu Group, lakini alitunga nyimbo zilizopendwa mno kwenye bendi ya Vijana Jazz Band.

Kalala, ambaye yeye pamoja na kupiga solo, ametunga nyimbo kama 'Maisha ya Amba', 'Stella', 'Chiapo',' Ilikuwa Lifti Tu', 'Penzi Halina Umaarufu, akiwa na Vijana Jazz, 'Nalila Masumanda', akiwa na Watunjatanjata na 'Baba Jeni' sehemu ya kwanza, ya pili na ya tatu, 'Ngondo Igwa', 'Vicky', na nyinginezo.

## Chausiku: Mcharuko uliopata bahati

**Na Adam Fungamwango**

WAZEE wa zamani hawakukosea kusema mtu anayependa, pengo huona mwanya na chongo huona kengeza. Mtu akipendacho hakina hila machoni. Huridhika kuwa nacho japo hakina thamani.

Penzi ndiyo kitu pekee ambacho kinaweza kumtoa tajiri Oysterbay, Masaki au Mbezi Beach na kwenda kulala Manzese au Tandale raha mstarehe.

Siku zote penzi halichagui. Na anayependa hata ukimuuliza ni kwa nini amependa hawezi kukupa jibu sahihi. Ni kwa sababu anayependa kufanya hivyo kutoka kwenye nyuma ya ubongo wake na uvunguni mwa moyo wake bila hiari yake.

Ndiyo maana mtunzi wa filamu hii ametoka na kitu kiitwacho 'Chausiku' Ni filamu itakayokuonyesha hiki kinachozungumzwa hapa.

Imecheza na baadhi ya wasanii mastaa kama Rammy Galls, Shamsa Ford, Hamisa Mobeto, Baba Haji na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa Rammy akiwa amerejea kutoka masomoni Marekani alikopelekwa na wazazi wake. Baada ya kumaliza masomo sasa wanamtaka aoe. Wakamtafutia msichana msomi mwezake Hamisa.

Angekubali kama asingekwenda uswazi kwenda kumsalimia rafiki yake wa zamani Haji. Huko alikutana na msichana mmoja wa uswazi, anaitwa Shamsa.

Rammy alitokea kumpenda Shamsa. Hata hivyo hawaendani naye. Shamsa ni binti wa kiswazi. Mkorofi. Ngumi nje nje. Kila siku kwenda kusuta wanawake wenzake na kuwabomoa. Ana mdomo utafikiri nini. Ni mcharuko hatari. Kwa vigodoro ndiyo usiseme.



Hata hivyo, Rammy anatokea kumpenda hivyo hivyo na hali yake jinsi alivyo akiwa na matgemeo kuwa atabadilika tu na kustaarabika mbele ya safari.

Tabia yake ya kuwa muongeaji sana kuliko kusikiliza, ndiyo ilimfanya hata wazazi wa Rammy kumkataa alipokwenda kumtambulisha.

Wazazi alimlaumu kijana wao kwa kuwaletea kituko ndani ya nyumba badala ya mchumba.

Wakamwambia hao wanamtaka Hamisa na si Shamsa. Wakamlazimisha Hamisa aje kwenye jumba lao la kifahari. Lakini hiyo haikuwa dawa ya Rammy kumchukua Hamisa. Kikubwa ni kwamba akamwambia ukweli kuwa yeye si chaguo la moyo wake. Anampenda mtoto wa uswahilini Shamsa ambaye alitumia jina la Chausiku kwenye filamu hiyo.

Pamoja na kupata aibu pindi alipokuwa akimtambulisha kwa wazazi, ndugu, jamaa na marafiki kutokana na hulka ya msichana mwenyewe kutokana na kutokuwa na elimu, pamoja na maneno yake yaliyoathiriwa na maisha ya uswahilini, hadi Rammy alizidi kumpenda.

Hali ilizidi kuwa mbaya. Penzi halilazimishwi. Mwishoni Hamisa na wazazi walivyoosha mikono juu kumruhusu Rammy amuoe Chausiku ambaye ni Shamsa.




# Atakayeligusa jina 'Omotola' kukiona

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Omotola Jalade-Ekeinde, wiki hii ametangaza kuliwekea hatimiliki jina lake kwa ajili ya kumnufaisha kibiashara.

Msanii huyo wa filamu aliyejizolea umaarufu nchini Nigeria, ameandika kupitia ukurasa wake wa Twitter kwamba jina lake "OMOTOLA" sasa lina hakimiliki.

Omotola amekuwa mwigizaji mwenye wafuasi wengi mtandaoni na ana ushawishi kupitia miradi yake mbalimbali ikiwamo vipindi vya televisheni.



## Kit, Rose wafurahia mtoto wao

WASANII wa filamu wa Marekani, Kit Harington na Rose Leslie, wamekuwa na furaha baada ya kupata mtoto wao wa kwanza tangu wawe mke na mume.

Kulingana na mtandao wa PageSix, waigizaji hao wa filamu ya 'Game of Thrones' wamepata mtoto wa huyo Februari 16, mwaka huu, wakiwa jijini London nchini Uingereza.

Wawili hao waliamua kuweka wazi uhusiano wao Septemba mwaka 2020, na kueleza wanatarajia kupata mtoto wakiwa pamoja.


## Michael B amzawadia Lori gari la kifahari

FEBRUARI 14 ambayo ilikuwa sikukuu ya wapendanao iliibua mshtuko kwa mastaa mbalimbali duniani, miongoni mwa staa aliyeshangaza mashabiki wake ni mwigizaji wa Marekani, Michael B. Jordan, ambaye alimzawadia mpenzi wake Lori Harvey, gari la kifahari aina ya Hermèr.

Kupitia Insta strori ya mwigizaji huyo, alionyesha stakabadhi ya manunuzi ya gari hilo kama zawadi ya Valentine.

"Mpenzi wangu nimefanya kitu kimoja kwako, itatusaidia kufanya matembezi binafsi na itakuwa kiunganishi kizuri kati yetu," ameandika.





## Nini kimemuua Decker?

KINARA wa filamu za Kinigeria, Victor Decker, amekutwa amefariki dunia akiwa ndani ya nyumba yake.

Kulingana na mashuhuda, mwili wa mwigizaji huyo ulikutwa ukiwa juu ya kochi baada ya kutoonekana kwa muda wa siku nne.

Majirani zake wamesema katika muda huo Victor hakuonekana ametoka ndani ya nyumba yake jambo ambalo liliwapa wasiwasi na kuamua kuripoti polisi.

## Paris Hilton achumbiwa tena

HATIMAYE mwanamitindo Paris Hilton, amevishwa pete ya uchumba kwa mara ya pili.

Bilionea huyo mwanamke amechumbiwa Februari 13, mwaka huu na Carter Reum.

Siku ya Jumanne, Hilton kupitia ukurasa wake wa Instagram ameonyesha pete yake hiyo na kueleza kwamba endapo ukitaka kufanya jambo, usitake kujua ila fikiria kwanza.



MAKALA

# JPM ammwagia sifa Balozi Kijazi

Na Ani Jozeni

- Alisimama pekee kutetea uadilifu, uzalendo
- Miundombinu Dodoma ndiyo iliyomwibua


Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli, akiongoza viongozi mbalimbali wa serikali kuaga mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi. **PICHA: IKULU PICHA: MTANDAO**

KIFO cha Katibu Mkuu Balozi John Kijazi, ambaye alikuwa mhandisi kwa taaluma na mwanadiplomasia kimajukumu, ni mmoja wa watu ambao wamefikia nafasi ya juu zaidi ya utumishi nchini bila kuingia katika siasa. Wakati amefariki, siku moja na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais huko Zanzibar, Seif Sharif Hamad, magazeti yalitofautiana habari ipi ni kubwa.

Kimsingi Maalim Seif aliteka mioyo ya wengi na majonzi ya kifo chake yalivuka mpaka, wakati Balozi Kijazi alifahamika zaidi serikalini, na siyo katika jamii ya Watanzania wengi, wanakojulikana zaidi wanasiasa.

Nafasi za Katibu Mkuu Kiongozi hapa nchini ni moja ya maeneo nyeti ila hayatajwi sana, na mara nyingine ni vigumu kusema wadhifa huo upo katika ngazi ipi serikalini, au katika taifa kwa jumla. Ni mtendaji mkuu katika utumishi wa umma.

Pia ndiye, mshauri mkuu kwa Rais kwa wasio wanasiasa, hali ambayo inahitaji utaalamu wa hali ya juu, kutumia taaluma ipasavyo katika kutoa ushauri, na huku mhusika akijua kuwa yeye si kiongozi wa kisiasa.

Nafasi yake hasa ni kumsaidia Rais, siyo kuwakilisha watu.

Ni jukumu analopewa mtu ambaye Rais anamwona kuwa ndiye mwaminifu na mwadilifu labda kuliko watumishi wengine aliona nao kwa sababu ambazo anakuwa amezishuhudia katika kipindi kilichotangulia. Ndiyo maana mara kadhaa Rais anahama na Katibu Mkuu wake katika wizara aliyokuwa kabla ya kuingia madarakani, au anateua mtu ambaye aliwahi kufanya naye kazi kwa karibu.

Ukaribu wa Rais John Magufuli na Balozi Kijazi ni katika kunyoosha utendaji serikalini, uadilifu na uwajibikaji na si urafiki.

Siyo rahisi kusema Katibu Mkuu Kiongozi ana mamlaka kiasi gani serikalini au ushawishi kwa nafasi yake, hasa kwa Rais kwani yuko naye muda wote awapo ofisini kwake.

Ila Rais Magufuli aliwahi kutoa kielelezo cha ushawishi huo akizungumzia ugumu wa kufanya mabadiliko serikalini, kwani watu wanakuwa na ulinzi wa ziada ambao wakuu wanaofanya mabadiliko wanaweza kuhisi kuwa kuna jambo ambalo si la kawaida kwa jinsi wanavyoendesha zoezi hilo. Alisema wakiwa wanajadili majina kufanya mabadiliko, alijisikia mchovu anahitaji kupumzika kidogo, akaenda muda mfupi na aliporudi, akakuta Balozi Kijazi naye imebidi akapate mapumziko kwa kujisikia vibaya kiasi fulani.

Kuna wakati Ofisi ya Rais ilikuwa na katibu maalum, na wakati wa awamu ya kwanza alikuwa Joseph Butiku, ambayo ni kama kugawa nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi iwe na maeneo mawili, lile la utawala wa kawaida kama mkuu wa utumishi serikalini, na msaidizi maalum wa masuala nyeti ya kiserikali.

> **Ukaribu wa Rais John Magufuli na Balozi Kijazi ni katika kunyoosha utendaji serikalini, uadilifu na uwajibikaji na si urafiki.**



Labda kinachofanya kumbukumbu ya Balozi Kijazi kuwa tofauti kiasi ni kuwa yeye ni mhandisi kwa taaluma na uendeshaji wa serikali ni jambo alilolifahamu kwa uzoefu, ila kutokana na mwelekeo huo wa kitaaluma aliendana vyema na mkuu wa nchia ambaye pia ni mwanasayansi kitaaluma.

Haina maana kuwa wanapokuwa wanasayansi kileleni kila kitu kitaenda sawa, lakini inawezekana kuna mchongo wa kisaikolojia wa wanasayansi.

Mfano ni miradi ya ujenzi awamu hii wakati aliyeko madarakani na msaidizi wake wa karibu zaidi walikuwa pamoja Wizara ya Ujenzi si kitambo sana, ambayo ina maana kuwa ni baraka kwa taifa hili watu hao walikutana wakaaminiana, wabuni mikakati.

Halafu kwa upande mwingine hata huko kujuana na kufanya kazi pamoja kwa mwelekeo wa dhati wa kitaaluma kunatokana na mazingira ya kisiasa ya kuingia madarakani awamu ya tano.

Kulikuwa na sintofahamu ndani ya CCM zilizoanzia mbali, makundi yakianza kusuguana nani atachukua nafasi ya urais awamu ya nne ikifikia kikomo.

Wanachama kwa upande wao wakisaka mrithi, lakini walio madarakani wakitafuta njia ya kuendelea na uongozi wa nchi bila kuvuruga chochote katika mpangilio bali hata safu ya utawala.

Wakati mwingine misimamo mikali iliendelea bungeni ambako vita vya uwajibikaji vilishamiri, vikafikia katika kuamua hatima ya watiania na CCM ikapata kingozi ambaye anaiongoza awamu ya tano.

Ilikuwa ndiyo njia pekee ya kuingiza madarakani serikali yenye uadilifu wa aina yake, ikiongozwa kitaaluma na watu waliokutana katika kilele cha ufanisi wa kazi, na siyo katika matayarisho ya kutwaa madaraka miongoni mwa makundi ya CCM. Siyo mazingira rahisi kuyarudia awamu hii ikifika kileleni, lakini hata kama wanasiasa wa kawaida watarudi madarakani wakiwa na kisasi cha 'kula bata' bado kazi za Balozi Kijazi akimsaidia Rais Magufuli kuibadili Tanzania zitang'ara muda mrefu katika historia ya nchi hii. Watakaokuja watawajibika kuzilinda, hata wasipobuni upeo mpya.

# Yanayopotosha watoto zama hizi



Watoto wanaposhiriki miziki ya singeli na burudani zisizo na maadili wanapotoka. Wazazi, walezi na jamii wasiruhusu mambo hayo ya kuwaangamiza yaendelezwe. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

WATOTO kujirusha kwenye vigodoro, kucheza singeli na kukimbilia kwenye vibanda umiza ni jambo linalopigiwa kelele na wadau wa malezi kwa kuwa ndiko kuangamia, lakini jambo ambalo halijashikiwa bango ni nyimbo zinazopotosha zinazoimbwa mubashara mitaani.

Kusikiliza nyimbo zenye mashairi yaliyojaa matusi, vijembe na maneno ya kejeli nako ni uwanja mpana unawoongezea mmomonyoko wa maadili kwa watoto wa taifa hili.

Wazazi na walezi wakumbuke kuwa tabia mbaya kama kuvuta bangi au kutukana matusi, kukataa shule na kujiingiza katika uhalifu si mambo pekee la kuwaangamiza watoto. Leo kuna mengi ya kufuatilia ikiwamo kushiriki kwenye nyimbo na kucheza muziki uliojaa ujumbe wa upotoshaji, vijembe, matusi, unyanyasaji na mambo ya faraghani.

Muziki na tungo zinazoimbwa leo na burudani zinazosikika kila mahali mijini na vijijini ni jambo ambalo watu wengi hawalijali, lakini ukweli ni kwamba linaathiri mwenendo wa maisha na mazingira yanayowazunguka watoto

> **Kwa hiyo haya yakomeshwe, vijiji na halmashauri zitunge sheria ndogo kukataza madudu hayo hadharani.**

tena zina mchango wa kuvuruga maisha yao.

Kwa mfano zipo ngoma za kienyeji huko mitaani hasa maeneo ya ukanda wa pwani mathalani kigodoro na kisingeli vinavyo haribu maadili ya watoto. Ni dhahiri binti ama kijana anayeishi kwenye mauzauza kama hayo kesho maisha yake yatakuwa yamejaa changamoto nyingi.

Atakuwa anazijua ngono kinadharia, kimatendo kwa kuwa anasikia na kuona mambo kama namwaga radhi, kusaula na matendo mengine mengi ambayo yangetakiwa kufanyika faraghani lakini huwekwa hadharani.

Kwa Dar es Salaam maeneo kama Tandale, Temeke, Manzese na Buguruni singeli, vigodoro, vibandaumiza, miziki ya kumwaga radhi mubashara na madudu mengine kama hayo si kitu kipya ni sehemu ya utamaduni hasa nyakati za sherehe na huchukuliwa kama sehemu ya burudani.

Burudani hizo zinaambatana na nyimbo zenye maneno ya kutukana, kuzungumzia na kuhamasisha matendo ya ngono, kusuta, kuna wengine wanacheza michezo ambayo haistahili kuonekana hadharani, mavazi yanayovaliwa yanapotosha maadili na kwa ujumla watoto wanaojazana kutizama au hata kucheza hatima yao au maisha yao ya kesho yamo kwenye kupotoka.

Ukifutatilia nyimbo na uchezaji wake mara nyingi upo kwa ajili ya kuamsha hisia za ngono pasipo kujali watizamaji au wasikilizaji wanaofuatilia hasa watoto wadogo.

Nyimbo hizo zinaposikilizwa na kutizamwa na watoto wadogo zinawajengea ujasiri wa kupotoka. Wapo wasichana wenye umri wa kuwa mama au mwanafunzi. Wanaposhiriki singeli, kutizama picha kwenye vibanda umiza na kucheza muziki huo mitaani wanapata ujasiri wa kuvua nguo, kuonyesha matiti na kufanya vituko ambavyo ni mmomonyoko mkubwa wa maadili.

Watoto wanajifunza kwa kuangalia na kusikiliza basi nao wanaanza kujengwa kitabia kama walivyomwona mama au dada au kaka anamwaga radhi kwenye kigodoro au singeli nao wanaondoka na somo hilo na kuendelea kutumbukia kwenye upotovu.

Hali hii inasababisha watoto kuanza ngono mapema, kuwa jeuri, kuwa na maneno na kauli za matusi, kutokujali na kuwa na ujuzi wa kutumia bangi, vilevi, kufanya ngono ututoni na matokeo yake ni kuharibikiwa kimaisha na makuzi na kusababisha kizazi cha watoto wasiokuwa na miiko wala maadili na wanaoshiriki kwenye ngono tena wasioheshimu hata wakubwa zao wakiwamo wazazi na walezi.

Nyimbo zinazoimbwa na uchezaji ngoma, kuangalia picha za ngono si tu kwamba kunawafundisha watoto ngono bali pia huwapa picha kuwa hivyo ndivyo wanavyopaswa kuishi katika jamii zao hata wakikua, hawawazi kuwaza kuwa kusoma shule ni kipaumbele badala yake wanafikiria njia bora ya kukwepa shule ili 'kujirusha' mitaani.

Watoto wanakuwa mafundi wa kutunga na kucheza ngoma ambazo mavazi yake hayapendezi, ni mabingwa wa kumwaga radhi, hawathamini shule wala kuangalia kinachoendelea darasani, kumbe bila kurekebisha hali hiyo ni wazi kuwa hata familia zao za baadaye nazo zitaharibika pia.

Nyimbo zinazoimbwa zama hizi ziwe mubashara mitaani, kwenye video, au uchezaji wa ngoma au vidogoro zinakwenda sambamba na maneno machafu au yanayofedhehesha kwa mfano hutaja viungo vya siri.

Maneno kama 'raha kupendwa na wewe' raha kuvua nguo ikiwamo dela, kubaki utupu na matamshi mengine kama 'mwanamke kiuno' ni mambo yanayotamkwa na watu wakiona wanawake wanamwaga radhi . Yote haya hufanywa mbele za watoto ambao ni wanafunzi bila kujali kuwa huyachukua maneno haya na kuanza kuyatumia popote kuanzia nyumbani, shuleni na mitaani.

Matokeo ya athari hizo ni pamoja na watoto wadogo wa chini ya miaka 10 kukatika hadharani na mbele za watu na huku wakivua nguo kama njia ya kufuata kile kaka na dada zao wanachowaambia au kuwaonyesha mitaani.

Kupitia singile au nyimbo zinazoimbwa mubashara mitaani watoto wanakuwa na fursa ya kujifunza maneno machafu ambayo si vyema kuyajua au hata kuyasikia.

Wazazi na walezi wanapoona watoto wanapotoka leo wasishangae nani kawafundisha watoto matusi. Ukweli ni kwamba mwalimu ni vigodoro, singeli mubashara mitaani na kazi za vibandaumiza. Jamii ndiyo iliyowaruhusu watoto hao kujifunza kwani imewapa ruhusa ya kushiriki mambo hayo yasiyo na maadili.

Michezo hiyo huambatana na ulevi, unaoamsha ngono, matokeo yake ni watoto kunyanyaswa kingono, kubakwa, kulawitiwa na kuambukizwa magonjwa na wengine kupata mimba ututoni. Wengine huachiwa maradhi kama UKIMWI na VVU au hata kuwaacha wakiandamwa na msongo wa mawazo kwa kile walichofanyiwa.

Kwa hiyo haya yakomeshwe, vijiji na halmashauri zitunge sheria ndogo kukataza madudu hayo hadharani. Ziundwe kamati za kulinda watoto mitaani, vijijini na popote wasiingizwe kwenye uharibifu huo na ufuatiliaji uwe endelevu.

HABARI KIMATAIFA

# Wanajeshi wafungwa baada ya kushambulia waandishi

**KAMPALA,** Uganda

MAHAKAMA ya Kijeshi ya Uganda imewahukumu kifungo cha siku 90 jela wanajeshi saba, baada ya kuwashambulia waandishi wa habari.

Wiki hii wanajeshi waliwashambulia waandishi hao wakiwa kazini wakiripoti tukio la Bobi Wine, akiwasilisha waraka kuhusu haki za binadamu katoka ofisi ya Umoja wa Mataifa (UN), nchini humo.

Jeshi la Uganda UPDF katika taarifa yake lilisema kamati ya nidhamu ya jeshi imewahukumu wanajeshi hao akiwamo ofisa wa cheo cha kapteni, pamoja na kuwapa onyo kali.

Ni nadra kwa walinda usalama nchini Uganda kuadhibiwa kwa kuwashambulia waandishi wa habari.

**Kwa bahati mbaya, kuna watu wachache walipata majeraha mkiwamo wanahabari. Tumeanzisha uchunguzi kujua ni katika mazingira gani waathirika walijeruhiwa.**

Matukio ya kushambuliwa waandishi yameongezeka katika miezi ya hivi karibuni hususan operesheni za kuwakamata wafuasi wa kiongozi wa upinzani Bobi Wine.

Jumatano wanajeshi walilivamia kundi la waandishi wa habari nje ya ofisi ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, na kuwapiga na waandishi 20 miongoni mwao wakijeruhiwa.

Ofisi ya UN nchini Uganda juzi ilisema Ofisi ya kamisheni ya haki za binadamu ilipata waraka huo kutoka kwa kiongozi wa upinzani Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine.

"Mwenendo huu unakiuka makubaliano na serikali, kukiangaziwa usalama wa majengo ya Umoja wa Mataifa, wafanyakazi na wageni," ofisi ya UN ilisema katika taarifa.

Polisi imesema maofisa wa usalama walitawanya umati usiodhibitiwa ambao ulikua umekusanyika nje ya ofisi ya Umoja wa Mataifa, wakati Bobi Wine akiwasilisha waraka huo.

"Kwa bahati mbaya, kuna watu wachache walipata majeraha mkiwamo wanahabari. Tumeanzisha uchunguzi kujua ni katika mazingira gani waathirika walijeruhiwa," Polisi iliema katika taarifa.

Waandishi wa habari 20 walijeruhiwa katika shambulizi hilo, na angalau wanne walikuwa na majeraha makubwa kichwani, katibu mkuu wa chama cha wanahabari wa Uganda, Stephen Bwire aliliambia Shirika la Habari la Reuters. **VOA/DW**



Maofisa wa kupambana na moto, wakizima moto uliotokana na mlipuko ndani ya gari katika eneo la viwanda mjini Bogota, Colombia juzi. **PICHA: REUTERS**

## Nusu ya Waafrika Kusini wadaiwa kuambukizwa COVID-19

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

INAKADIRIWA vifo vinavyohusiana na uganjwa wa COVID-19 ni karibu asilimia 0.4 nchini Afrika Kusini.

Kulingana na ripoti mbalimbali watu 120,000 wamekufa kutokana na ugonjwa huo, na kwamba zaidi ya watu milioni 30 wameambukizwa virusi vya corona, sawa na karibu nusu ya wakazi wa nchi hiyo.

Makadirio hayo ni sawa na utafiti wa kingamwili, ambao unabaini kwamba kati ya asilimia 32 na 63 ya raia wa Afrika Kusini wameambukizwa virusi tangu kuzuka kwa janga hilo nchini humo.

Uwepo wa kingamwili kwenye damu unaweza kugundua ikiwa mtu ameambukizwa virusi hata baada ya kupona.

Utafiti uliochapishwa wiki iliyopita na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Damu (South African National Blood Service) ulifanywa kupitia jopo la watu 5,000 waliojitolea kutoa damu katika majimbo manne tu ya nchi hiyo.

Afrika Kusini inapitia wimbi la pili la COVID-19, ambayo husababishwa na aina mpya ya kirusi cha corona kinachojulikana kuwa kinaambukiza zaidi.

Hivi karibuni, idadi ya kesi mpya zilifikia karibu 2,000 kwa siku, dhidi ya zaidi ya 20,000 mwishoni mwa Desemba, mwaka jana.

Nchi hiyo ilizindua kampeni yake ya chanjo Jumatano ikiitumia kutoka kampuni kubwa ya dawa ya Marekani Johnson & Johnson.

Kulingana na gazeti la kila siku la Mail & Guardian, hata waganga wa jadi watahusika katika kampeni ya chanjo. **RFI**

# Bunge lavunjwa nchini Algeria

**Algiers,** ALGERIA

RAIS wa Algeria, Abdelmadjid Tebboune ametangaza kulivunja Baraza la Wawakilishi na kuitisha uchaguzi haraka.

Abdelmadjid Tebboune alitangaza mabadiliko ya Baraza la Mawaziri katika muda wa saa 48 zijazo wakati wa hotuba ya televisheni juzi usiku.

"Nimeamua kuvunja Baraza la Wawakilishi na kuitisha uchaguzi mpya ili kuweka taasisi mpya," alitangaza bila kutoa tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi huo.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walichaguliwa mwaka 2017, wakati washirika wa Abdelaziz Bouteflika, mtangulizi wa Abdelmadjid Tebboune, wakiwa wengi katika baraza hilo.

Abdelmadjid Tebboune alisema uamuzi huo ni sehemu ya mageuzi yenye lengo la kutoa nguvu zaidi kwa bunge.



Katika hali ya kutuliza mvutano wa kisiasa Rais Abdelmadjid Tebboune alitoa msamaha kwa wanaharakati zaidi ya 50 wa vuguvugu la Hirak.

Hatua hiyo iliwahusu hasa watu 30 waliohukumiwa mapema wiki hii kifungo cha hadi miaka miwili jela.

Rais hajataja majina, aliahidi kwamba kati ya watu 55 na 60 watajiunga na familia zao kuanzia leo.

Anatoa msamaha huo kwa watu hao siku chache kabla ya maadhimisho ya pili ya kuanzishwa kwa vuguvugu la Hirak. **RFI**

## Ethiopia yalaumu Sudan ghasia mpakani

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

SERIKALI ya Ethiopia imeishutumu Sudan kuchochea mgogoro kati ya mataifa mawili ambayo yamekuwa katika mvutano wa mpaka.

Ghasia ziliibuka mwishoni mwa mwaka jana kuhusu eneo la wakulima wa Ethiopia ambalo Sudan inadai ni eneo lake. Pande zote mbili zimekuwa zikishutumiana kwa kusababisha ghasia.

Mvutano umekuja wakati Ethiopia ikiwa na mgogoro Kaskazini mwa ukanda wa Tigray.

Katika taarifa kali iliyotolewa na serikali ya Ethiopia, imelishutumu Jeshi la Sudan kuchochea mvutano huo kuingia kwenye vita.

Licha ya kudai mzozo huo kuhusiana mvutano wa eneo la wafugaji walioko karibu na mpaka, inaonekana masuala ya kisiasa kuhusika pia.

Taarifa ya Ethiopia ilisema Jeshi la Sudan linachochea mgogoro ili kuinufaisha Misri.

Kumekuwa na mvutano mkubwa kati ya Ethiopia na serikali ya Misri juu ya ujenzi wa bwawa katika Mto Nile. **BBC**

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yoyote zaidi yao. Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani?

Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kukufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane-9

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**

Safari yao iliishia kaunta, ambako walitakiwa kwanza kuwasilisha vitu walivyonavyo kwa ajili ya kukaguliwa.

“Samahani kwa sasa tumeambiwa ni lazima tusachi kwanza pochi, mikoba na vitu wanavyobeba wanaingia kwenye vyumba kwa sababu wengine wanakuwa na silaha, au vitu vya kuhatarisha wenzao, si mnakumbuka lile sakata la mtu kuuawa na mpenzi wake gesti lilivyotikisa?” Dada mmoja wa kaunta alisema huku akichukua mkoba wa Mwanaidi kwa ajili ya upekuzi.

Ni maneno yaliyomshtua Mwanaidi. Mwili wake ulitetemeka. Lakini hakuna yoyote aliyetambua hilo.

“Laiti angetambua kuwa anayemsema ni mimi?” Mwanaidi alijisemea kimoyomoyo.

Mwanaidi wakati mwingine huwa hapendi kabisa kukumbuka, au kukumbushwa tukio hilo ambalo limegharimu ustawi wa maisha yake, kiasi cha kutokuwa na amani na ndilo limezaa hadi hili la pili la kutakiwa kuua.

Dakika moja baadaye alimrudishia na kuwakabidhi chumba. Kazi ilienda kama ilivyopangwa.


Tika alizidiwa na kinywaji. Kitu ambacho kilikuwa kinamuudhi zaidi Mwanaidi ni kupapaswa na mwanaume huyo. Hata hivyo alilazimika kukubali kwa ajili ya kutimiza jambo lake.

Hakutaka yafikie mwisho. Hakutaka ifikie hatua ya kulala na mwanaume huyo. Hivyo kitendo bila kuchelewa, alisubiri ameingia msalani ulio humo humo chumbani, aliingiza mkono kwenye mkoba wake na kutoa dawa alizoambiwa. Vilikuwa ni vidonge viwili ambavyo alivitumbukiza haraka kwenye glasi aliyokuwa akinywa Tika.

Aliporudi hata hakuongea kitu, aliichukua glasi iliyokuwa na nusu bila, akaimimina kinywani.

Dakika 15 tu baadaye, Tika alikuwa anakoroma na kutoa mapovu kinywani.

Alikusanya vitu vyake na kuondoka taratibu. Lengo ilikuwa akimbie mji. Lakini akakumbukua kuwa polisi walimtaka asitoke nje ya mkoa wa Dar es Salaam kutokana na mauaji ya mpenzi wake Burhan.




Kwa hili lililotokea, aliaambiwa na Martin kuwa atamlinda kwa gharama yoyote ili asijulikane kama ni yeye ndiye aliyefanya hivyo. Kutokana na hilo hakudhani kuwa polisi watajua kama ni yeye aliyefanya hivyo kwa sababu hata alivyojipamba na kuvaa wigi, alifanya kila njia ili kujibadilisha mwonekano. Ni siri kati yake na Martin tu.

Pia alikumbuka kuwa kuna malipo ya pesa ambayo aliahidiwa kutokana na alichokifanya.

Badala ya kukimbia, akaamua kurejea nyumbani kwake Mburahati kwa ajili ya kumsubiri Martin.

**************************

Saa mbili baadaye wakati Mwanaidi akiwa ameshajibwaga kitandani akitafakari kilichotokea mlango uligongwa. Alitarajia hilo. Alimtarajia mgeni huyo. Hakuwa na wasiwasi alikwenda kufungua.

Kama alivyotarajia, mgeni alikuwa ni Martin. Aliingia ndani huku akitabasamu. Mwanaidi alikuwa amepanga chumba na varanda.

“Twende chumbani.” Aliamuru Martin.

Kwa jinsi hali ilivyotokea huko walikotoka, Mwanaidi aliona ni kweli mazungumzo yanatakiwa yafanyike chumbani.

Moja kwa moja Mwanaidi alikaa kitandani akimruhusu mgeni wake akae popote anapopataka ili asikilize atakachokisema na sana sana kumpa mzigo wake wa pesa kutokana na kazi chafu aliyoifanya ya kumuua Tika.

Ilikuwa imetimia saa saba na nusu usiku. Dunia yote ilikuwa kimya. Chumbani, Mwanaidi alikuwa amewasha taa ya balbu yenye rangi ya bluu kwa ajili ya kulalia, hivyo kuufanya mwanga kuwa hafifu kidogo.

“Tayari Martin, nimeshamaliza kazi, nipe changu basi.” Alisema Mwanaidi kwa sauti ndogo.

Martin bado alikuwa amesimama. Ghafla aliingiza mkono mfukoni na kutoa bastola.

Akafuatia na kucheka kicheko cha dharau. Hali ile iliyotokea ghafla ilimtisha mno Mwanaidi.

Hakutarajia kukutana na hali ile kwa wakati ule. Sasa tayari alijiona mfu. Alijuta kwenda kumfungulia mlango.

“Kwanza nashukuru kwa kazi kubwa uliyoifanya ya kumuua yule kinyago Tika.”

Martin aliongea kwa kujiamini na kuonekana kabisa kuwa amebobea kwenye mambo ya ukatili.

Mwanaidi aliligundua hilo baada ya kudanganywa na kupelekwa kwenye ofisi yake, alipopewa maagizo ya kwenda kuua, lakini hakujua kuwa ni katili zaidi ya alivyofikiria.

“Niliposema zawadi yako, sikuwa na maana kuwa ni pesa. Zawadi pekee utakayopata Mwanaidi ni kifo.” Ni maneno yaliyotoka kwa Martin, yakimtisha Mwanaidi kuliko kifo chenyewe.

“Umeua. Halafu uendelee kuishi. Kwenye kanuni ya ujambazi, kama wewe siyo jambazi haikubaliki. Nikikuachia unaweza siku yoyote kama siyo leo hata miaka kumi ijayo ukatoa siri.

Nimekutumia wewe kwa sababu niliona ni rahisi kufanya hivyo, kuliko nigefanya vingine.” Alisema huku akichezea bastola yake. Hakuwa na haraka sana ya kumnyooshea kwa sababu aliyekuwa naye pale ni mtoto wa kike. Aliitoa kwa sababu ya kumtisha na kumuharibu kisaikolojia.

Mwanaidi alikuwa ni kama anaota ndoto. Ndoto mbaya ya jinamizi. Hakuweza kunyanyua mdomo na kuongea lolote kwa wakati huo.

“Labda alikuwa hujui kitu. Mimi hapa unavyoniona, ndiye mkuu wa kundi la majambazi liitwalo ‘Black Cobra’ ambao mpenzi wako Burhan alikuwa mwanachama.

Huyu mpumbavu Tika uliyemuua leo, nilitaka afe kwa sababu moja tu. Ananidai pesa nyingi ambazo sitaki kumpa. Huyu ndiye aliyenipa ramani ya kwenda kupora gari linalosambaza pesa kwenye ATM. Ni mfanyakazi wa benki, amenipa kila kitu muda na aina ya gari, namba zake, idadi ya pesa zitakazopelekwa, idadi ya askari waliolisindikiza na silaha watakazotumia.

Kazi hiyo ilifanywa na bwana ‘ako Burhan na wenzake, sasa huyu naye anataka mgao wake. Mgao ni huo ameupata.” Alisema huku akitabasamu na kuangalia Mwanaidi ambaye alimuona Martin kama ziraili mwenyewe mtoa roho.

Sasa Mwanaidi ndipo alipotambua kuwa mpenzi wake marehemu Burhan alikuwa jambazi na kweli zile pesa alizoziona siku ile zilikuwa ndiyo zile zile ambazo alikuwa ametoka kuzipora kwenye gari la kusambazia pesa kwenye matawi ya kuchukua pesa kwa mashine ATM.

“Kumbuka kuwa Mwanaidi una kesi ya kumuua huyo mpenzi wako, si ndiyo?” Aliitikia kwa kichwa.

“Na pesa ukachukua zaidi ya milioni mia moja?” Hakujibu kitu.

Martin akaangua kicheko cha dhihaka, kilichozidi kuchanganya Mwanaidi.

“Sikiliza Mwanaidi, una kesi mbili sasa za mauaji. Ya kwanza ni kumuua mpenzi wako Burhan, ya pili ni kumuua Tiika, mfanyakazi wa benki. Sasa mimi nimeona nikusaidia kitu kimoja tu. Nikutandike risasi ya kichwa ili uzikwepe kesi hizi zote mbili. Kumbuka kesi moja tu inatosha kabisa kukutia kitanzi.”

Ghafla ujasiri wa ajabu ukamjia Mwanaidi, akajikuta maneno yakimtoka kinywani.

“Naomba unisamehe Martin. We uniache tu mimi na kesi zangu. Hata kama nitanyongwa huko mbele ya safari sawa tu, lakini kwa sasa naomba unisameke.”

“Nikusamehe ukawaambie polisi kuwa nimekutuma kwenda kumuua Tika?”

“Siwaambii?”

“Hata kama hukuwaambia. Watafanya uchunguzi na watakubaini na wewe utawaambia kuwa ni mimi. Ili mimi niwe salama ni lazima wewe ufe. Hata kama wakijua ni wewe tayari utakuwa umeshakuwa marehemu, hivyo uchunguzi utaishia hapo. Watajua kuwa aliyemuua Tika ni Mwanaidi. Mwanaidi yule yule aliyemuua mpenzi wake Burhan, kwisha.”

Machozi yalimtoka Mwanaidi. Hakuwa na tumaini lolote sasa la kubaki hai. Kuna wakati aliona ni bora risasi ipenye kwenye kichwa chake ili akapumzike kutokana na kesi mbili za mauaji, moja imeshaanza kumkabili na nyingine itamkabili baadaye.

Lakini siku zote kifo hakizoeleki, woga wa kufa unamwingia na kuona ni bora aendelee kuwa hai ili apambane na kesi hizo.

Hata hivyo akiangalia sura ya Martin hakuona dalili yoyote ya yeye kubaki hai.

Aliongea maneno ambayo hakutoka mdomoni. Ndiyo kwa mara ya kwanza akaanza kujuta kukutana na Burhan.

Ni Burhan tu ndiye aliyemletea matatizo yote haya. Pamoja na kumpenda na pesa nyingi alizompa, lakini kazi yake ya ujambazi ndiyo imeletea kupata kesi zote mbili za mauaji.

“Mimi nadhani nisipoteze muda Mwanaidi. Sikupenda kukuua mtoto mzuri kama wewe. Lakini nimelazimika kufanya hivyo. Kwa heri. Nenda kamsalimie Burhan mpenzi wako mwenyewe ambaye ukaamua kumuua kwa ajili ya zile milioni mia moja zilizokuwa kwenye mfuko wake.” Alisema huku mkono wake ukinyooka kutaka kumfyatulia risasi Mwanaidi.

***Itaendelea Jumamosi***



# SPURS

## SASA IMEAMKA UPYA - MOURINHO

**BUDAPEST, Hungary**

JOSE Mourinho anatambua ushindi wa Tottenham wa 4-1 dhidi ya Wolfsberger haukuwa "rahisi", lakini amesisitiza utaleta mtazamo chanya kwa kikosi chake.

Son Heung-min, Gareth Bale, Lucas Moura na Carlos Vinicius kila mmoja alifunga bao moja katika mchezo huo uliopigwa mjini Budapest Alhamisi, wakati Spurs wakijiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kufuzu hatua ya 16 kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Europa.

Huo ulikuwa ni ushindi wa pili kwa kikosi cha Mourinho, katika mechi zake saba zilizopita kwenye mashindano yote.

"Tulikuja na kucheza kwa malengo na tumefanikiwa. Tulitakiwa kufunga mabao zaidi ya 3-0 kipindi cha kwanza," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Kipindi cha pili tulifanya makosa na yakawafanya wao kuamka. Ilikuwa ni sawa kama ilivyokuwa kwenye mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Everton.

"Kama unatawala mchezo halafu baadaye unafanya makosa, unampa mpinzani wako nafasi kubwa ya kurudi mchezoni.

"Tulitawala vizuri mchezo. Tulikuwa na nafasi nyingi. Naamini bao la mwisho lilitufanya tujiamini zaidi. Ushindi wa 4-1 ugenini ni matokeo mazuri sana."

# SARE YA ARSENAL YAMTIBUA ARTETA

**ROME, Italia**

MIKEL Arteta ameonya Arsenal lazima "ipambane" ili kupata matokeo baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Benfica kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Europa raundi ya 32 pale katika dimba la Olimpico, juzi Alhamisi mjini Rome.

Bukayo Saka alisawazisha dakika mbili tu baada ya Pizzi kufunga kwa penalti na hivyo halikutosha kuwawezesha Arsenal kupata pointi zote tatu.

Pierre-Emerick Aubameyang alikosa nafasi kadhaa za kufunga na sasa kocha wa Arsenal, Arteta anaona kikosi chake kina nafasi ndogo ya kufuzu hatua inayofuata.

Mchezo wa marudiano utapigwa katika dimba la Georgios Karaiskakis mjini Athens nchini Ugiriki Alhamisi ijayo.

**"Tulitawala sana mchezo na kutengeneza nafasi ny ingi," alisema akiiambia BT Sport. "Tunatakiwa kupambana sana.**

"Ni matokeo ya kukatisha tamaa kwa namna tulivyoruhusu watufunge bao. Tuliwapa mchezo rahisi na wakatufanya tutoke 1-1.

# LIVERPOOL YAJIPANGA KUMSAJILI RAPHINHA

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool sasa imeamua kuingia sokoni kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake baada ya kukumbwa na majeruhi.

Kwa mujibu wa Daily Mail Liverpool wanataka kumsajili winga wa Leeds United, Raphinha mwenye umri wa miaka 24.

Taarifa zinaeleza kuwa Liverpool imeshafanya mazungumzo binafsi na mchezaji huyo raia wa Brazil na wanapanga kumsajili wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Nyota huyo amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwa kikosi cha Leeds na hivyo kuzivutia klabu kadhaa kuwania saini yake.

Liverpool imekuwa na majeruhi wengi msimu huu na hata nafasi yake ya kutetea taji la Ligi Kuu England ipo shakani, ikiwa inashika nafasi ya sita kwenye msimamo.

Lakini pia 'Wekundu' hao wa Anfield wanaivizia saini ya kiungo wa Udinese, Rodrigo de Paul mwenye umri wa miaka 26, baada ya kushindwa kumsajili katika dirisha dogo la Januari.



# RUDIGER

## SASA ATAKA MKATABA MPYA CHELSEA

**LONDON, England**

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger, amedokeza kuwa anataka kusaini mkataba mpya pale Chelsea.

Nyota huyo wa zamani wa Roma alipata changamoto ya kupata muda wa kucheza akiwa chini ya Frank Lampard, lakini tangu kuwasili kwa kocha, Thomas Tuchel, amekuwa aking'ara katika safu ya ulinzi.

Beki huyo wa kati alibaki Stamford Bridge kwa madirisha mawili ya hivi karibuni ya uhamisho licha ya kuhusishwa na kuhamia kwingine, na kwa kuwa mkataba wake wa sasa unafika mwisho 2022, inaonekana ametuma ujumbe kwa uongozi wa Chelsea unaonesha kuwa anataka kubaki.

Akizungumza na Sky Sports News, Rudiger alisema: "Ndani mwangu, nilikuwa mtulivu kila wakati na niliyetulia, nitakuwa mwaminifu sana. Sikuwa nikicheza mwanzoni na wakati haupo kwenye kikosi, unajiuliza, ni nini kinachotokea?

"Lakini ghafla nilikuwa nimerudi kwenye timu na kupata michezo kadhaa. Kuanzia wakati huo, nilijiambia kichwani 'Ninasalia hapa Chelsea na ninajaribu kupigania nafasi yangu'. Katika michezo ya mwisho ya Frank Lampard, nilikuwa nacheza mara nyingi zaidi."

Rudiger amecheza dakika 90 kamili katika mechi sita za mwisho za Chelsea za Ligi Kuu, pamoja na zote nne tangu Tuchel achukue hatamu katika timu hiyo yenye makazi yake mji mkuu wa Uingereza, London.

# Sarri awapiga vijembe Juventus, Ronaldo

**TURIN, Italia**

KOCHA wa zamani wa Juventus, Maurizio Sarri, amewaponda waajiri wake wa zamani baada ya mwendelezo wa matokeo mabovu ya klabu hiyo.

"Inafurahisha sana kuwaona Juventus katika nafasi hiyo (nafasi 4). Waliniambia kwamba nilikuwa nikifundisha mpira mbovu zaidi, lakini nilimaliza wa kwanza kwenye ligi na nikawafanya washerehekee ubingwa," alisema Sarri.

"Sasa itafurahisha zaidi kuona jinsi Cristiano Ronaldo atachukua hatua wakati huu wakati labda atalazimika kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

"Wakati wangu nikiwa kocha wa Juventus alikuwa wa kwanza kuiambia bodi ya timu kwamba alikuwa hana furaha nami baada ya kuondoshwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Halikuwa kosa langu, lakini kosa lao kwa sababu walikuwa wakicheza na mimi nilikuwa pembeni.

"Labda bodi yake ya Juventus haitamsaliti na tuone jinsi wanavyofanya kwenye Ligi ya Mabingwa mwaka huu. Wacha tuone ni nani aliye sawa," aliongeza Sarri.




# Henry kuinoa Bournemouth

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry, anaongoza katika mbio za kuwania nafasi ya kuwa kocha mpya wa Bournemouth.

Kwa mujibu wa gazeti la Mirror Sport, bodi ya klabu hiyo inapendekeza nguli huyo wa Arsenal mwenye umri wa miaka 43, ili kumrithi Jason Tindall aliyefukuzwa kazi wiki mbili zilizopita.

Nafasi ya kocha katika timu hiyo kwa sasa iko wazi na Henry anapewa nafasi kubwa dhidi ya kocha wa zamani wa Huddersfield, David Wagner.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES ANACHOTAKA NI MATAJI TU MAN UNITED

●●●Kucheza bila kubeba kitu fulani haisaidii, mpira wa miguu unapocheza maana yake unatafuta...

**TURIN, Italia**

BRUNO Fernandes ameshauri wachezaji wenzake wa Manchester United "kukua na kupambana" dimbani ili kuongeza nafasi ya kushinda mataji, baada ya kung'ara kwenye mchezo wa ushindi wa Ligi ya Europa dhidi ya Real Sociedad, juzi, Alhamisi.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno alifunga mara mbili kabla ya Marcus Rashford na Daniel James kufunga moja moja na kuiwezesha Man United kuibuka na ushindi wa mabao 4-0 pale kwenye dimba la Allianz mjini Turin nchini Italia.

Fernandes sasa amehusika katika mabao 52 kwenye mashindano yote tangu alipoanza kuichezea United Februari mwaka jana, 10 zaidi ya mchezaji yeyote wa Ligi Kuu kwa kipindi hicho.

Ushindi huo sasa unawaweka 'Mashetani Wekundu' hao kwenye nafasi nzuri ya kufuzu hatua ya 16 katika mashindano hayo.

Na Fernandes anataka kushinda taji lake la kwanza akiwa na Man United tangu alipoondoka Sporting CP, ambako walipoteza kwenye nusu fainali tatu msimu wa 2019-20.

"Tunatakiwa kuimarika na kucheza kwa kujituma zaidi uwanjani, la msingi ni kupambana zaidi," alisema Fernandes akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Leo (juzi) tumecheza kwa kuelewana sana, naamini kila mechi tukicheza vile tuna nafasi kubwa ya kupata ushindi na hivyo ndivyo inavyotakiwa.

"Mimi nataka tuongeze ari zaidi ili tuweze kushinda mataji, kucheza bila kubeba kitu fulani haisaidii, mpira wa miguu unapocheza maana yake unatafuta kitu na sisi huu ndio wakati wetu.

"Tukiongeza nguvu ya kupambana uwanjani, tutakuwa na nafasi kubwa kupata taji msimu huu, na hilo ndio muhimu sana kwangu."

## KWA UFUPI

**RODRIGUEZ KUONDOKA EVERTON**

STRAIKA wa Everton, James Rodriguez, mwenye umri wa miaka 29 raia wa Colombia, anafikiria kuondoka hapo Goodison Park licha ya kutua kipindi cha majira ya joto kilichopita. ***(Defensa Central)***

**SULE AWANIWA CHELSEA**

CHELSEA inataka kumsajili mlinzi wa Bayern Munich na Ujerumani, Niklas Sule mwenye umri wa miaka 25. ***(AZ)***

**MADRID WAKOMAA NA MBAPPE**

REAL Madrid imewekeza nguvu na mipango yake katika kuhakikisha wanamsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufarannsa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22. ***(AS)***

**POCHETTINO KUMBAKIZA MBAPPE**

KOCHA wa PSG, Mauricio Pochettino, amesema klabu hiyo inaweza kumpa kile anachotaka Kylian Mbappe ili kumfanya awe na furaha na abakie hapo. ***(Catalunya Redio, via RMC Sport)***

**TUCHEL AMTAKA HOFMANN**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, pia anafikiria kumsajili kiungo wa Borussia Monchengladbach na Ujerumani, Jonas Hofmann, mwenye umri wa miaka 28. ***(Bild)***

**ODEGAARD HAUZWI- MADRID**

REAL Madrid haitamuuza kiungo wake, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, ambaye anacheza kwa mkopo kule Arsenal, lengo likiwa ni ili aweze kumvutia raia mwenzake wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye miaka 20 kutua hapo, akitokea Borussia Dortmund. ***(Mundo Deportivo)***

**HENRY ANUKIA BOURNEMOUTH**

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry, anaweza kuthibitishwa kuwa kocha mpya wa Bournemouth wiki ijayo. ***(Mirror)***

**SON NA MKATABA MPYA**

STRAIKA wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min, amesema "sio sawa kuzungumza kuhusu mkataba mpya". Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 raia wa Korea Kusini, unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2022-23. ***(Sun)***

**JUVENTUS YAMTAKA KEAN**

JUVENTUS itajaribu kumsajili tena mshambuliaji wa Everton na Italia, Moise Kean mwenye umri wa miaka 20, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo kule PSG. Toffees hao walimsajili Kean kutoka Juve mwaka 2019. ***(Le 10 Sport)***

**EVERTON YAMWANIA VAZQUEZ**

EVERTON ina nia ya kutaka kumsajili winga wa Real Madrid, Lucas Vazquez. Winga huyo raia wa Hispania mwenye umri wa miaka 29, pia anawaniwa Napoli. ***(Todofichajes)***

**AARONS KUONDOKA NORWICH**

NORWICH City ipo tayari kumpoteza mlinzi wake wa pembeni mwenye umri wa miaka 21, Max Aarons kwa klabu kubwa. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

# KOCHA AZAM FC ABAINI WANAPOJIKWAA LIGI KUU

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mbeya City juzi, bado Azam FC inakazi kubwa ya kuhakikisha inaendelea kufanyia kazi kasoro zilizopo kikosini ikiwamo kuruhusu mabao kirahisi kwa mujibu wa Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Vivier Bahati.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex juzi usiku, mabao ya wenyeji yalifungwa na Iddi Selemani `Nado` dakika ya tano na Prince Dube aliyepachika bao la pili dakika ya 30 huku la kufutia machozi kwa Mbeya City likifungwa na David Mwasa dakika ya 69.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Bahati alisema mechi hiyo ilikuwa na ushindani mkubwa, lakini wachezaji wao walizembea baada ya kuona wanaongoza mabao 2-0 kipindi cha kwanza na kufanya makosa yaliyotoa nafasi kwa wapinzani wao kupata bao hilo moja.

Alisema hayo ni makosa ambayo yanaanzia kwa wachezaji wote na si suala la safu ya ulinzi pekee.

"Huwezi kuwalaumu mabeki kwamba tatizo liko kwao, ni wachezaji wote hasa tunapokuwa tunaongoza kipindi cha pili kwetu kinakuwa na presha kubwa kwa wapinzani wetu, hii imejitokeza katika mechi mbili ikiwamo dhidi ya Simba, Coastal Union na leo (juzi) dhidi ya Mbeya City," alisema Vivier.

Alisema wanaendelea kufanyia kazi tatizo hilo na ana imani katika mechi ijayo hawatauruhusu bao kizembe kama ilivyo kwenye mechi hizo tatu za mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Kwa ushindi huo, Azam imefikisha pointi 36 ikiwa katika nafasi ya tatu huku Yanga ikiendelea kutesa kileleni na alama zake 46 wakati huu mabingwa watetezi, Simba wakiwa nafasi ya pili na pointi 42 na mechi mbili mkononi za kiporo.



Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Alhaji Rajabu Kundya (katikati aliyevaa kaunda suti ya mikono mirefu) akiwa pamoja na viongozi mbalimbali na baadhi ya wachezaji wa timu ya riadha watakaoshiriki mbio za Kilimanjaro Marathoni zitakazofanyika Februari 28, mwaka huu, mjini Moshi, wakati alipotembelea kambi yao katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU). **MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaridhishwa maandalizi Kili Marathon 2021

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeridhishwa na maandalizi ya mbio za mwaka huu za kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zinazotarajiwa kufanyika Jumapili ya wiki ijayo mjini Moshi, imeelezwa.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Alhaj Mwangi Kundya, wakati alipotembelea kambi ya wanariadha wa Kitanzania watakaoshiriki mbio hizo iliyoko Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Serikali inafuatilia kwa karibu masuala yote ya kiusalama ya kiafya kwa manufaa ya wananchi wetu kila siku ikiwamo siku ya mbio hizo maarufu, inatia moyo kuona kuwa waandaaji wa mbio hizo wamechukua tahadhari za kutosha hii inatia moyo," alisema.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na waandaaji wa mbio hizo pamoja na wadhamini wake mbalimbali ili kuhakikisha usalama wa kiafya wa washiriki wote kwa njia moja au nyingine.

Aidha, aliwashukuru wote waliofadhili kambi hiyo ambapo alisema ni hatua mojawapo ya kuhakikisha wanariadha wa Tanzania wanafanya vema kwenye mbio hizo za mwaka huu zinazotarajiwa kufanyika katika Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU).

"Serikali imeweka mikakati kabambe yenye lengo la kukuza michezo hapa nchini ukiwamo mchezo wa riadha ili kulilitea heshima taifa kupitia sekta ya michezo, nachukua fursa hii kuwapongeza waandaaji wa mbio za Kilimanjaro Marathon kwa kuziendeleza kila mwaka," alisema.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mwenyekiti wa Chama cha Riadha mkoani Kilimanjaro (KAAA), Adrma Mikumi, alisema tahadhari za kiafya zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka maji tiririka kwenye maeneo yote ya Uwanja wa Ushirika, pamoja na watu watakaokuwa na vitakatishi (sanitizers) kwa ajili ya wale watakaofika uwanjani siku hiyo.

"Ili kuepuka misongamano ya watu kwenye maeneo ya kunawia mikono pamoja na kupulizia vitakatishi, kutakuwa na watu ambao jukumu lao litakuwa ni 'kusanitize' watu ili wasisongamane eneo moja ikiwa ni sehemu ya tahadhari," alisema na kuongeza kuwa washiriki wote na watazamaji watapewa barakoa za kutumika kabla na baada ya kukimbia wanapokuwa katika mkusanyiko.

Aidha, alisema pia kutakuwa na maji tiririka yenye dawa maalum kila kituo kinachohusika na mbio hizo ambako wakimbiaji watapitia ili kuhakikisha usalama wa washiriki wa mbio hizo.

Kwa upande wake Makamu wa Rais wa Chama cha Riadha nchini (RT), John Bayo, aliwatoa hofu washiriki na wananchi wengine baada ya kueleza kuwa tahadhari hizo hazimaanishi kuwa kuna changamoto yoyote ya kiafya.

"Barakoa zitakazotolewa haimaanishi kuwa kuna changamoto yoyote ya kiafya bali ni tahadhari tu maana Tanzania haiko kwenye kisiwa na pia kutakuwako na wageni wengi hivyo tahadhari ni muhimu sana haswa ikitiliwa maanani serikali pia imeshatoa angalizo kwa wananchi wachukue tahadhari za kiafya kama inavyoelekezwa na wataalamu wa afya," alisema Bayo, ambaye ndiye Mkurugenzi wa mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager.

Mbio za mwaka huu zimedhaminiwa na bia ya Kilimanjaro Premium Lager-kwa zile za kilomita 42, Tigo wamedhamini mbio za kilomita 21(Half Marathon) wakati Grand Malt wamedhamini mbio za kilomita tano.

Wadhamini wa vituo vya kunywa maji (water table) ni Unilever Tanzania, Simba Cement, TPC Sugar, Kilimanjaro International Leather Company Limited, Kibo Palace Hotel na watoa huduma maalumu ni Garda World Security, Keys Hotel na CMC Automobile huku zikiandaliwa na Kilimanjaro Marathon Company Limited na kitaifa zikiratibiwa na Kampuni ya Executive Solutions Limited.

## Coastal nguvu sasa kwa JKT Tanzania

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya Jumatano wiki hii kukubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji FC katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, benchi la ufundi la Coastal Union limesema kwa sasa linaelekeza nguvu zake kumulika pointi tatu itakaposha uwanjani hapo kesho dhidi ya JKT Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Juma Mgunda, alisema makosa ambayo ameyabaini katika mchezo uliopita dhidi ya Dodoma Jiji anaendelea kuyafanyia kazi na anaimani atayamaliza kabla ya kuivaa JKT Tanzania kesho.

"Mchezo uliopita wachezaji wangu walifanya uzembe mpaka tukafungwa, nitafanyia kazi vizuri makosa hayo kabla ya kesho," alisema Mgunda. Alisema anawapa wachezaji wake mazoezi maalumu ambayo yatawasaidia kufanya vizuri katika mechi zao zijazo ikiwamo huo wa kesho huku akiwataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuwapa ushirikiano pasipo kukatishwa tamaa na matokeo yaliyopita.

Aidha, alisema anaupa umuhimu mkubwa mchezo wao huo kwa kile alichoeleza kuwa JKT Tanzania ni moja ya timu yenye wachezaji wazuri.

## KVZ yatoa sababu kushindwa kufurukuta

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa timu ya KVZ, Sheha Khamis, amesema kupoteza baadhi ya michezo katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar, kulitokana na kikosi chake cha kwanza kuandamwa na majeruhi wengi.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema kikosi chake kiliandamwa na majeruhi karibu katika kila mechi waliyoshuka dimbani hali iliyosababisha baadhi ya michezo kutofanya vizuri.

Alisema tathmini ya timu yake katika mzunguko huo wa kwanza uliomalizika timu ilifanya vizuri licha ya nafsi ya ushambuliaji kuonekana kuwa na tatizo kidogo.

"Licha ya kuwa na majeruhi wengi, lakini bado kuna tatizo kwenye nafasi ya ushambuliaji, katika michezo tuliyocheza utaona nafasi nyingi za wazi ambazo tunatengeneza zinashindwa kuzaa matunda," alisema.

Akizungumzia mzunguko ujao wa lala salama ambao awali ulipangwa kuanza leo kabla ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kuahirisha ili kupisha maombolezo ya msiba wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, kocha huyo alisema matarajio yake ni kuona wanafanya vizuri na kuunyakuwa ubingwa wa Zanzibar.

Timu ya KVZ ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 20 zilizotokana na mechi 11.

# Michezo

Jumamosi Februari 20, 2021

Nipashe




FERNANDES ANACHOTAKA NI MATAJI TU MAN HABARI UK 22

NAWAKERA...



Winga wa Simba, Bernard Morrison, akifanya vitu vyake dhidi ya mabeki wa Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara ambayo aliifungia timu yake bao pekee wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA YAITANGAZIA AL AHLY 'TOTAL WAR'

## ●●●Yasema kichapo lazima, Waarabu wachachawa watua nchini saa sita usiku, Bwalya na Mkude nao warejea...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kaulimbiu ya "War in Dar" kufanya kazi dhidi ya FC Plataínum na kuiwezesha Simba kushinda na kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, klabu hiyo sasa imekuja na kaulimbiu mpya ya "Total War" (Vita Kamili) ikichagizwa na 'The Point of No Return' (Hakuna kurudi Nyuma), hiyo ikiwa ni maalum kwa ajili ya mechi yao dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Katika mechi ya raundi ya kwanza kuwania kutinga hatua ya makundi, Simba ilikubali kipigo cha bao 1-0 ugenini nchini Zimbabwe dhidi ya FC Platinum, na iliporejea jijini Dar es Salaam, ilitangaza kaulimbiu ya 'War in Dar' kueleka mechi ya marudiano ambayo ilifanya kazi kwa kushinda 4-0 na kutinga hatua ya makundi.

Na wakati huu Simba ikitarajiwa kuikaribisha Al Ahly katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumanne kwenye mechi yao ya pili ya hatua ya makundi ikiwa ni baada ya kushinda mchezo wa kwanza ugenini kwa bao 1-0 dhidi ya AS Vita ya DR Congo, lakini Waarabu hao wa Misri nao wakishinda 3-0 nyumbani dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan, mabingwa hao wa Tanzania wametangaza kaulimbiu ya 'Total War' kwa ajili ya mchezo huo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema mechi hiyo ni muhimu sana na wachezaji watapambana kupata pointi tatu katika mchezo huo kutokana na maandalizi waliyofanya na dhamira waliyokuwa yao. "Hii ni mechi kubwa sana, ukizingatia Al Ahly si 'level' (daraja) ya chini, ila tukiwa na jambo letu basi hakuna kurudi nyuma, hivyo hii ni Total War (Vita Kamili), isiyo ya silaha wala kuumizana, tumejipanga kuhakikisha wapinzani wetu hawatoki Tanzania.

"Hii ni vita ndani ya uwanja, tunahitaji kupata pointi tatu muhimu, nimeongea na wachezaji na kutuhakikisha wanaingia katika mapambano kupata ushindi," alisema Manara.

Alisema wanaiheshimu Al Ahly ni Mabingwa wa Afrika, lakini Simba wanahitaji kufanya vizuri katika mechi zao kwa sababu nao wanahitaji kufika katika daraja hilo la wapinzani wao hao, huku akiongeza kuwa tayari wachezaji sita waliokuwa wamekwama DR Congo wamesharejea na kuungana na wenzao kambini. "Wachezaji ambao walikwama DR Congo wamefika jana na tayari wameungana na wenzao kambini tayari kwa mechi yetu ya Jumanne," alisema.

Wachezaji hao ni Jonas Mkude, Rally Bwalya, Erasto Nyoni, Kennedy Juma, Ally Salim na Meneja wa timu Abasi Ally.

Manara alitaja viingilio vya mechi hiyo kuwa mzunguko ni Sh. 3,000, VIP B, Sh. 15,000 na VIP A Sh. 30,000 na kwamba siku ya mwisho kuuza kwa bei hiyo itakuwa Jumatatu saa sita usiku na baada ya hapo atakayenunua siku ya mechi alazimika kutoa Sh. 5,000, 20,000 na 40,000. **Wakati huo huo**, Manara alisema kwa wapinzani wao Al Ahly walitarajiwa kutua nchini jana saa sita usiku kwa ajili ya mchezo huo, ambao unatarajiwa kuwa mgumu kwa kila upande huku akimtaja mgeni rasmi wa mchezao huo kwamba atakuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Damas Ndumbaro ambaye atakuwa miongoni mwa vigogo watakaoshuhudia mchezo huo.

**Katika hatua nyingine** Manara alishangaa kuona watani zao, Yanga kila Bernard Morrison anapocheza na kuifungia Simba, kuibuka na kuanza kuibua sakata la kesi zake, huku akiipongeza serikali na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kusimamia vema soka la Tanzania.

## YANGA YAIBUKA NA WAAMUZI, MORRISON

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka sare tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga leo kwa mara nyingine inatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar, huku uongozi wa klabu hiyo ukitishia kujitoa kwenye ligi kutokana na kile walichodai kutotendewa haki na waamuzi, lakini ikilitupia lawama Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa kutowaita kusikiliza malalamiko kuhusu dosari za mkataba wa Simba na Bernard Morrison.

Yanga inaingia uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Kagera Sugar Jumatano iliyopita na kusababisha taharuki kubwa kutoka kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Akizungumza jana kwenye mkutano na waandishi wa habari, Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema wamekuwa na mechi nyingi ngumu, lakini maamuzi upande wao yanakuwa si mazuri, hivyo sasa wanatafakari kama waendelee kuwapo au wajitoe.

"Kesho (leo), tunategemea kuwa na mechi. Tunaamini kabisa kuwa haki itakuwapo. Kama haitokuwapo, sisi kama Kamati ya Utendaji tutaamua vinginevyo juu ya ushiriki wetu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Kwa nini matukio haya yanatokea kwenye mechi za Yanga tu? Maamuzi yanakuwa si mazuri kwa upande wetu. Sasa tunajiuliza hii ligi tuendelee kuwapo au tujitoe," alisema Mwakalebela.

Makamu Mwenyekiti huyo alirejea kwenye mechi dhidi ya Mbeya City na ile ya Kagera Sugar, akidai kuna uonevu mkubwa unaofanywa na waamuzi dhidi ya timu yake na kulitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi kuliangalia suala hilo na kuchukua hatua stahiki.

Kuhusu Morrison, alisema wamepeleka malalamiko yao TFF, kuhusu kuwapo kwa dosari za mkataba wake na Klabu ya Simba lakini hadi leo shirikisho hilo halijawaita kuwasikiliza.

Pamoja na hayo, Mwakalebela amewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa watulivu na kuendelea kushikamana na viongozi wao, kwani amedai huenda kuna njama za kuwafanya wafarakane na kwa ajili ya kufifisha azma yao ya kutwaa ubingwa msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002